**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

---

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

# SERA YA TAIFA YA UFUGAJI NYUKI

**DAR-ES-SALAAM**
**MACHI, 1998**

Kimepigwa chapa na KIUTA Dar es Salaam - Tanzania

# SERA YA TAIFA YA UFUGAJI NYUKI

**DAR-ES-SALAAM**
**MACHI, 1998**

# YALIYOMO

**UKURASA**

**YALIYOMO ………………………………………………………………………………………..… iii**

**DIBAJI………………………………………………………………………………………………..…… vi**

**VIFUPISHO………………………………………………………………………………………………… viii**

**FAHARASA ………………………………………………………………………………………….… ix**

**1. MFUMO WA KITAIFA WA UUNDAJI WA SERA YA UFUGAJI NYUKI……………………… 1**

1. 1 Mfumo wa Jumla Kiuchumi…………………………………………………………………………… 1

1.2 Mfumo wa Kimazingira……………………………………………………………………….. 2

1.3 Mfumo wa Kijamii……………………………………………………………………………… 4

**2. MATATIZO MAKUBWA YALIYOPO KISEKTA NA FURSA ZILIZOPO……………………. 5**

2.1 Usimamizi wa Rasilimali za Nyuki na Mimea ya chakula chao kwa ajili ya maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii na uboreshaji wa Mazingira…………………………… …... 5

2.1.1 Uwezo uliopo wa kuzalisha mazao ya Nyuki………………………………………… . 5

2.1.2 Mchango wa Ufugaji Nyuki Katika Maendeleo ya Kijamii, Kiuchumi na Uhifadhi wa Mazingira…………………….. …………………… .. . 5

2.1.3 Ufugaji Nyuki huboresha uhifadhi wa Bioanuwai……. ………………………………. 6

2.2 Matatizo Yanayokwamisha Maendeleo ya Sekta ya Ufugaji nyuki……………………… 6

2.2.1 Kutokuwapo kwa Sera na Sheria za Ufugaji nyuki………………………………… 6

2.2.2 Kukosekana kwa Uratibu Rasmi wa masuala ya Sekta ya Ufugaji Nyuki kati ya Sekta hiyo na Sekta zinazohusiana za Misitu, Kilimo na Wanyamapori…………… 7

2.2.3 Kukosekana kwa Huduma Madhubuti za Ugani wa Ufugaji Nyuki……………….. 9

2.2.4 Ukosefu wa Takwimu za kutosha za kuwezesha kupanga Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Ufugaji Nyuki……………………………………………………….. 9

2.2.5 Ukosefu wa Vifaa vya Kutosha na vinavyofaa kuchakatia na Kuhifadhia Mazao ya Nyuki………………………………………………………………… . 10

2.2.6 Ukosefu wa Huduma za Usafirishaji kwa ajili ya shughuli za Ugani na Mazao ya Nyuki……………………………………………………………… 10

2.2.7 Kukosekana kwa masoko ya kuaminika ya Mazao ya Nyuki…………………… .. 10

**3. LENGO NA MADHUMUNI YA SEKTA YA UFUGAJI NYUKI…………………………… 10**

**4. MATAMKO YA SERA……………………………………………………………………… 11**

4.1 Uanzishaji na Usimamizi endelevu wa Hifadhi za Nyuki………………………………… .. 11

4. 1. I Hifadhi za Nyuki za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa…………………………. 11

4.1.2 Hifadhi za Nyuki za Watu Binafsi………………………………………………… 12

4.2 Usimamizi wa Manzuki……………………………………………………………… 13

4.2.1 Manzuki za Serikali………………………………………………………………… 13

4.2.2 Manzuki za Binafsi……………………………………………… ………………… 13

4.3 Viwanda vinavyojikita kwenye shughuli za Ufugaji Nyuki na Mazao ya Nyuki…………… 14

4.3.1 Vifaa vya Ufugaji Nyuki…………………………………………………………… 14

4.3.2 Viwanda na Bidhaa Zitokanazo na Asali…………………………………………… 15

4.3.3 Viwanda na Bidhaa zitokanazo na Nta……………………………………………… 16

4.3.4 Viwanda na Bidhaa zitokanazo na uchavushaji……………………………………… 16

4.3.5 Viwanda Vingine Vinavyotegemea Bidhaa za Nyuki………………………………… 17

4.3.6 Utalii wa Kiikolojia………………………………………………………………… 17

4.4. Ufugaji Nyuki Katika Maeneo ya Sekta Mtambuka………………………………………… 18

4.4.1 Ufugaji Nyuki Katika Ardhi huria……………………………………… ………… 18

4.4.2 Ufugaji Nyuki Katika Maeneo ya Kilimo…………………………………………….. 19

4.4.3 Ufugaji Nyuki Katika Mapori ya Akiba……………………………………… …… 19

4.4.4 Ufugaji Nyuki Katika Hifadhi za Taifa………………………………… …………… 20

4.4.5 Ufugaji Nyuki Katika Misitu ya Hifadhi na Mashamba ya Miti………………………… 21

4.5 Ufugaji Nyuki katika Kuhifadhi na Kusimamia Mifumo Ikolojia……………………………… 21

4.5.1 Usimamizi wa Viuwadudu………………………………………………………… 21

4.5.2 Ukadiriaji wa Athari kwa Mazingira………………………………………………… 22

4.6 Asasi na Nguvukazi……………………………………………………………………… 22

4.6.1 Mfumo wa kupanga, kutekeleza na kuratibu shughuli za Ufugaji Nyuki……………… 22

4.6.2 Mfumo wa Kisheria na Udhibiti…………………………………………………….. 23

4.6.3 Utawala katika Sekta ya Ufugaji Nyuki……………………………………………… 25

4.6.4 Serikali za Mitaa………………………………………………………………………… 26
4.6.5 Utafiti wa Ufugaji Nyuki……………………………………………………………….. 26
4.6.6 Mafunzo na Elimu ya Ufugaji Nyuki………………………………………………………. 27
4.6.7 Huduma za Ugani wa Ufugaji Nyuki………………………………………………………. 28
4.6.8 Vyama vya Ushirika na Jumuiya nyinginezo za Wafugaji Nyuki…………………………..29
4.6.9 Biashara ya Mazao ya Nyuki……………………………………………………………. 29
4.6.10 Mashirika Yasiyo ya Kiserikali……………………………………………………….. 30
4.6.11 Masuala ya Fedha…………………………………………………………………… 30
4.6.12 Jumuiya ya Kimataifa……………………………………………………………………32

**5. DHIMA NA MAJUKUMU YA WASHIKADAU WAKUU……………………………………….33**

**DIBAJI**

Sekta ya ufugaji nyuki Tanzania imeendeshwa bila ya kuwa na sera tangu mwaka 1949 wakati ilipoanzishwa rasmi kama idara katika Wizara ya Kilimo. Tangu wakati huo, mwongozo wa kuendeleza na kusimamia rasilimali za nyuki na mimea ya chakula chao umekuwapo kupitia maagizo ya kitaalamu na kiutawala. Madhumuni makuu ya mwongozo huo yalikuwa ni kuufanya ufugaji wa nyuki uwe wa kisasa kwa kuanzisha mizinga ya masanduku, kuongeza uzalishaji wa asali na nta na kuongeza mapato yatokanayo na uuzaji wa asali na nta nchi za nje .

Mabadiliko mengi ya kijamii, kiuchumi na kimazingira yanayotokea pamoja na marekebisho ya sera kuu ya uchumi yaliyotekelezwa nchini, na ongezeko la kujali uhifadhi wa mazingira ili kuleta maendeleo endelevu ya ufugaji nyuki yamepelekea kuundwa kwa Sera ya Ufugaji Nyuki. Sera hii inazingatia nafasi ya ushirikiano na uratibu wa sekta mtambuka ambao utaimarisha usimamizi endelevu wa rasilimali za nyuki na mimea ya chakula chao katika mashamba ya kilimo, misitu na maeneo ya wanyamapori yaliyohifadhiwa.

Rasimu ya sera ya ufugaji nyuki awali ilitayarishwa kama sehemu ya Sera ya Misitu na utayarishaji wa rasimu hii ulihusisha washikadau husika katika warsha tatu tofauti, mikutano mbali mbali ya Idara ya Misitu na Nyuki, Washauri wa Kitaalamu na kikosi maalumu cha utekelezaji. Rasimu ya mwisho ilitayarishwa kwa kuboresha na kuunganisha hoja, mapendekezo na maazimio yaliyopitishwa na warsha hizo tatu na katika mikutano mingine ya kiushauri.

Chanzo kingine muhimu cha habari zilizotumika katika rasimu hii ya mwisho ni Mpango wa Utekelezaji wa Misitu Tanzania (TFAP) ambao unajumuisha Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (NBP). Masuala muhimu yanayohusu maendeleo ya sekta ya ufugaji nyuki yaliyokuwamo katika Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ambayo yalitayarishwa mwaka 1989 yakiwahusisha washikadau wakuu katika mikutano ya vijiji na warsha za kitaifa, yamejumuishwa katika sera hii. Iliamuliwa kuwa rasimu inayojitegemea ya Sera ya Ufugaji Nyuki iandikwe badala ya kuijumuisha na ile ya Misitu, ili malengo na madhumuni yake yawe bayana na yenye kueleweka. Hii pia inatazamiwa kuwa itawezesha kuzingatiwa kikamilifu kwa masuala ya sekta ya ufugaji nyuki na yale ya sekta mtambuka zenye misingi yake katika ufugaji nyuki na matamko ya sera ambayo ndiyo msingi wa uundaji wa Sheria ya Ufugaji Nyuki. Sheria ya Ufugaji Nyuki itakuwa ndiyo nyenzo kuu ya utekelezaji wa sera hii.

Sera ya Ufugaji Nyuki ambayo lengo lake kuu ni kuimarisha mchango wa kudumu wa sekta hii kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi na uhifadhi wa mazingira, inajumuisha kwa pamoja nyuki wanaouma na wasiouma, bila kujali masuala ya umiliki na usimamizi. Sera inahusu pia makundi ya nyuki wasiofugwa na wale wanaofugwa pamoja na nyuki wengine ambao hukusanya mbochi (nectar) au chavua (pollen) kama chakula chao.

**VIFUPISHO**

| | |
|---|---|
| EIA | Ukadiriaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira |
| FAO | Shirika la Chakula na Kililmo la Umoja wa Mataifa . |
| FBD | Idara ya Misitu na Nyuki |
| GDP | Pato la Taifa |
| HMF | Hydroxy-methyl-Furfuraldehyde |
| MNRT | Wizara ya Maliasili na Utalii |
| NBP | Programu ya Kitaifa ya Ufugaji Nyuki |
| NBRC | Kituo cha Njiro cha Utafiti wa Ufugaji Nyuki |
| NFP | Programu ya Taifa ya Misitu |
| NGO | Shirika lisilo la Kiserikali |
| PSRC | Tume ya Rais ya Kurekebisha Sekta ya Umma |
| RPFB | Mpango Unaoendelea na Bajeti ya Upeo |
| SWRI | Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori ya Serengeti |
| TAFORI | Taasisi ya Utafiti ya Misitu Tanzania |
| TFAP | Mpango wa Utekelezaji wa Misitu Tanzania |
| UNCED | Kongamano la Kimataifa la Mazingira na Maendeleo |

**FAHARASA**

**Kilimo Misitu -** Huu ni mtindo wa kilimo ambapo mazao na miti huoteshwa na kustawishwa kwa pamoja ndani ya shamba moja.

**Ufugaji Nyuki-Kilimo Misitu** – Ni mtindo wa kilimo ambapo mazao na miti huoteshwa na kustawishwa kwa pamoja ndani ya shamba moja, kwa ajili ya nyuki wanaouma na wasiouma ili wakusanye mbochi (nectar) na chavua (pollen) kutoka kwenye maua na wakati huo huo, kutoa huduma ya uchavushaji wa mimea hiyo.

**Manzuki (Shamba la Nyuki)** – Ni eneo lenye makundi ya nyuki yanayomilikiwa.

**Utawala wa Sekta ya Ufugaji Nyuki** – Unahusisha serikali ya Tanzania katika suala la usimamizi na uendelezaji wa shughuli za ufugaji nyuki chini ya Idara ya Misitu na Nyuki.

**Vifaa vya Ufugaji Nyuki** – Inajumuisha mizinga, patasi ya mzinga, mavazi ya kinga, bomba la moshi, chujio za asali na nta, vifaa vya kuhifadhia nta na asali na vifaa vya kuchakatia na kupimia viwango vya asali na nta.

**Mazao ya Nyuki** – Inajumuisha asali, nta, chavua, gundi ya nyuki (Propolis), maziwa ya nyuki (Royal jelly), majana ya nyuki, nyuki hai na huduma za uchavushaji.

**Hifadhi ya nyuki** – Hii ni sehemu maalum iliyowekwa kwa makusudi ya kuendeleza rasilimali ya nyuki na mimea ya chakula chao.

**Kundi la Nyuki** – Ni jamii ya nyuki wa asali yenye malkia mmoja, maelfu ya nyuki vibarua, na makumi au mamia ya nyuki dume. Kundi hili lina uwezo wa kujigawa na kupata makundi mawili au zaidi yanayojitegemea kibiolojia.

**Kipindi cha uchavusho** – Ni kipindi ambacho nyuki na maua vinahitajiana. Kipindi hiki mbochi na chavua hupatikana kwa kiasi kikubwa na uwezekano wa uchavusho ni mkubwa zaidi.

**Taasisi ya Utekelezaji** – Hii ni taasisi ya kibiashara itakayojiendesha yenyewe na ambayo itaundwa kwa madhumuni ya kusimamia hifadhi za nyuki au manzuki za maonyesho kwa ajili ya shughuli za Kiugani. Wafanyakazi katika taasisi hii wataajiriwa na serikali ambapo mikataba na masharti ya ajira zao vitafafanuliwa na taasisi hiyo.

**Nyuki Mwitu** – Ni makundi ya nyuki ambayo hayamilikiwi na mtu yeyote.

**Nyuki wasio vimelea** – Inajumuisha nyuki wanaotafuta au kukusanya mbochi na chavua ambayo hutumika kuwalisha majana ya nyuki badala ya chakula kinachotokana na wadudu wengine.

**Nyuki vimelea** – Inajumuisha nyuki wanaolisha majana yao kwa kutumia chakula kitokanacho na wadudu, yaani hulisha majana yao nyuki wa aina nyingine, mchwa, mbawakau na viluwiluwi vya wadudu wengine.

# 1. MFUMO WA KITAIFA WA UUNDAJI WA SERA YA UFUGAJI NYUKI

## *1. 1 Mfumo wa Jumla Kiuchumi*

Tangu mwaka 1986 Tanzania imekuwa ikifanya mageuzi ya kisera na kitaasisi ambayo madhumuni yake ni kuinua uchumi wa taifa. Mageuzi haya yameleta mabadiliko ya mazingira ya uchumi kwa kiasi kikubwa. Madhumuni ya kiuchumi na kijamii na Sera kama ilivyoelezwa kwenye Mpango Unaoendela na Bajeti ya Upeo (RPFB 1996/97-1998/99) ni kama yafuatayo:

- Kupiga vita umasikini na ufukara ili kuboresha hali ya maisha ya wananchi;
- Kuhakikisha uimara wa uchumi wa jumla;
- Kudumisha maendeleo endelevu kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira;
- Kuweka mazingira mazuri ili kuwa na sekta binafsi iliyo imara;
- Kupunguza ushiriki wa serikali kwenye shughuli za uzalishaji mali;
- Kuinua ufanisi katika matumizi ya rasilimali za Taifa.

Programu Kabambe ya mageuzi katika sekta ya fedha inaandaliwa na inatazamiwa kuwa muhimu katika kuhamasisha maendeleo ya shughuli za sekta binafsi. Hii pia itahusisha mageuzi kwenye benki zinazomilikiwa na umma. Tume ya Rais ya Kurekebisha Sekta ya Umma tayari imepitisha mpango wake kabambe wa urekebishaji wa sekta ya umma ambapo mashirika ya umma 128 yalitazamiwa kubinafsishwa au kufilisiwa. Lengo kuu ni kuboresha matumizi ya rasilimali chini ya uongozi na/au umilikaji mpya kwa matarajio ya kuinua kiwango cha ufanisi katika sekta ya fedha.

Shughuli kuu za serikali zitatazamwa upya ambapo zile za uzalishaji zitapungua ama kwa kujiendesha kibiashara au kwa kubinafsishwa na serikali itaelekeza nguvu zake kwenye sekta nyeti tu. Vivyo hivyo, zoezi la kupunguza watumishi wa serikali litafanyika ili kuipa uwezo serikali kuwalipa ujira wa kuridhisha watumishi watakaobaki. Lengo jingine la mageuzi kwenye mfumo wa ujira ni kuweka utaratibu wa mfumo mzuri wa ujira na wa uwazi zaidi.

Mazingira mazuri yatawekwa kwa ajili ya kukuza sekta binafsi na maendeleo ya kibiashara yatapewa msukumo. Hatua zilizochukuliwa kisera ni pamoja na kutohoa Sera ya Taifa ya kukuza uwekezaji, soko huria kwa mazao ya chakula na biashara, ushirikishwaji wa watu binafsi kwenye mashirika ya umma na uanzishwaji wa benki binafsi. Vile vile mkakati maalum wa misaada utawekwa ili kuhakikisha kuwa programu zote zinazohisaniwa kutoka nje zinaendeshwa kwa ufanisi zaidi na programu hizo zinakuwa endelevu. Jitihada zitafanyika kuhimiza uanzishwaji wa viwanda vidogo na vya kati kwa lengo la kuongeza uzalishaji, kukuza ajira na kukuza maendeleo ya viwanda vijijini. Upatikanaji wa mikopo na fedha za kigeni utaboreshwa kwa kuanzisha taasisi mpya za mikopo. Mazingira mazuri yatawekwa kwa ajili ya ushirikishwaji wa sekta binafsi katika uwekezaji na uzalishaji. Uendelezaji wa nguvukazi utaimarishwa ili kuhakikisha ufanisi wa uendeshaji wa viwanda.

### *1.2 Mfumo wa Kimazingira*

Sera ya kitaifa ya mazingira inaainisha mfumo wa sera ya mazingira; sera ambayo ni muhimu kwa sekta nyinginezo zinazohusiana nayo, ikiwemo ile ya ufugaji nyuki. Malengo ya jumla ya sera ya taifa ya mazingira ni kama yafuatayo:

- Kuhakikisha upatikanaji, ulinzi na matumizi sawa ya rasilimali kwa ajili ya mahitaji muhimu ya vizazi vya sasa na vijavyo bila ya kuharibu mazingira au kuhatarisha afya au usalama wa binadamu;
- Kuzuia na kudhibiti uharibifu wa ardhi, maji, mimea na hewa ambavyo ndivyo vinashikilia mifumo ya maisha yetu;
- Kuhifadhi na kuimarisha urithi wetu wa asili, na usio wa asili, ikiwa ni pamoja na bioanuwai zilizo katika mfumo wa kiikolojia wa kipekee wa Tanzania;
- Kuboresha hali na uzalishaji wa maeneo yaliyoharibiwa ikiwa ni pamoja na makazi ya vijijini na mijini ili Watanzania wote waweze kuishi katika mazingira safi, mazuri, yenye tija na yanayoridhisha kiuchumi-
- Kuongeza utambuzi na ufahamu wa uhusiano kati ya mazingira na maendeleo, na kuendeleza ushirikishwaji wa watu binafsi na jumuiya katika masuala ya mazingira; na
- Kukuza ushirikiano wa kimataifa katika agenda ya mazingira na kupanua ushirikishwaji na kutoa mchango kwa mashirika na programu baina ya pande mbili, kikanda na kimataifa ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa mikataba.

Kuna uhusiano tegemezi kati ya umaskini na uharibifu wa mazingira. Uharibifu wa mazingira huchangia katika kuleta umaskini uliokithiri na vivyo hivyo umaskini ni chanzo sugu cha uharibifu wa mazingira. Hivyo, haja ya kujitosheleza kwa mahitaji ya msingi ya binadamu ni jambo la kuzingatiwa katika Sera ya Mazingira. Uwekezaji katika ufugaji nyuki ambao ni chanzo cha kuaminika cha mapato na ambacho hakiathiri vibaya mazingira, ni muhimu katika kulinda mazingira kwa sababu mazingira ni muathirika wa kwanza kutokana na umaskini uliokithiri, msongamano wa watu mijini, ufugaji holela, kupungua kwa ardhi inayofaa kwa kilimo na ukame.

Uharibifu wa mazingira unaathiri vibaya rasilimali ya nyuki na mimea ya chakula chao ambavyo ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya ufugaji nyuki.

Umilikaji wa ardhi na maliasili (zikiwemo Hifadhi za Nyuki na Manzuki) na haki ya kutumia rasilimali hizo ni muhimu sana, siyo tu kwa kuleta uwiano wa kimaendeleo bali pia kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira. Ni pale tu watu wanapoweza kukidhi mahitaji yao, kudhibiti na kulinda rasilimali na kuwa na uhakika wa kumiliki ardhi, ndipo ambapo malengo ya muda mrefu ya uhifadhi wa mazingira yatakidhiwa. Umilikaji wa pamoja wa ardhi inayosimamiwa na halmashauri za vijiji unatoa mazingira mazuri ya kisheria kwa maendeleo ya misitu ya jamii, usimamizi wa Hifadhi za Nyuki na Manzuki na uendelezaji wa mifumo ya Ufugaji Nyuki-Kilimo Misitu.

Sayansi na teknolojia vina umuhimu mkubwa katika utumiaji wa maliasili na athari za matumizi hayo kwa mazingira. Lengo la msingi ni ukuzaji wa teknolojia ambazo haziharibu mazingira; yaani teknolojia zinazolinda mazingira, zisizotoa uchafu mwingi, zinazotumia rasilimali kiendelevu, zinazorejeleza takataka na masazo na ambazo zinatumia mabaki kwa namna inayokubalika. Matumizi ya teknolojia zisizoharibu vibaya mazingira katika ufugaji nyuki zinajumuisha:

- Mabomba ya moshi ambayo yakitumika wakati wa kuvuna/kurina asali yanaepusha uchomaji moto mapori;
- Mavazi ya kinga yanayofaa ambayo humlinda mfugaji asiumwe na nyuki na vilevile kuwalinda nyuki wasife;
- Mizinga mbadala ya ile inayotengenezwa kutumia magome ya miti ambayo inapelekea miti kufa.

Tanzania ni moja ya nchi kumi na nne duniani zenye bioanuwai nyingi. Programu za kuhifadhi na kutumia bioanuwai ili kudhibiti upoteaji mkubwa wa bioanuwai hizo zitatekelezwa. Sera, mikakati na programu za uhifadhi wa bioanuwai na matumizi endelevu ya rasilimali za biolojia na jene zitajumuishwa katika sera, mikakati na programu husika za kisekta mtambuka.

Ukadiriaji wa Athari kwa Mazingira ni chombo kitumikacho kusaidia katika utoaji wa maamuzi ili kuhakikisha kwamba hasara na uharibifu wa mazingira unaepukwa. Kama sehemu ya utekelezaji wa sera ya mazingira, miongozo na vigezo mahsusi vya ukadiriaji wa athari kwa mazingira vitaundwa.

Usimamizi wa mazingira ni jukumu la kila mtu. Majukumu makubwa ya taasisi za serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali ni kuisaidia jamii kwa kuwapa mwamko kuhusu hali yao na kuwaunga mkono ili wawajibike ipasavyo. Mambo muhimu yanayohitajika ili yapatikane maendeleo endelevu ni ushirikishwaji kikamalifu wa jamii katika ukadiriaji na utoaji wa maamuzi kuhusu athari kwa mazingira yanayogusa makazi yao na sehemu za kazi.

Sekta binafsi, hasa katika biashara na viwanda, inaweza kuchangia sana katika kupunguza shinikizo kwenye matumizi ya rasilimali na mazingira. Shughuli za kibiashara na viwanda zina wajibu wa kuboresha mifumo ya uzalishaji kwa kutumia teknolojia na njia zenye utumiaji wa kiufanisi zaidi wa rasilimali unaotoa uchafu kidogo, kuongoa, kurejeleza na kutumia tena bidhaa zitokanazo na uzalishaji huo. Sekta binafsi na jumuiya za mashirika yasiyo ya kiserikali zinatoa mtandao wa kitaifa ambao ni budi utumiwe, kuwezeshwa na kuimarishwa ili kuunga mkono juhudi za kufikia malengo ya kimazingira. Nafasi ya wanawake katika shughuli zinazohusiana na mazingira zitaendelezwa ili kuongeza ushiriki wao katika maeneo kama vile ya misitu, ufugaji nyuki, kilimo, na programu za usimamizi wa masuala ya maji.

### *1.3 Mfumo wa Kijamii*

Kujiondoa kwa serikali kwenye shughuli za uzalishaji kutawezesha kupatikana kwa rasilimali nyingi zaidi kwenye sekta ya huduma za jamii. Msisitizo mkubwa utawekwa kwenye mamlaka za ngazi za chini ili kuimarisha ushiriki wa jumuiya katika kutoa na kusimamia huduma za kijamii kwa njia ya kuchangia. Lengo kuu la sekta ya elimu ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2000 elimu ya msingi inapatikana kwa wote kupitia mgawanyo wa madaraka na ulegezaji wa masharti katika huduma hiyo. Sekta binafsi na wananchi watahimizwa kushiriki kwa mapana zaidi kwenye maendeleo na usimamizi wa elimu ya juu. Lengo la sekta ya afya ni kutoa huduma ya afya kwa watu wote na msisitizo utakuwa zaidi kwenye afya ya msingi na ya kinga kwa jamii. Ushiriki wa wananchi, mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na sekta binafsi kwenye sekta ya afya utatafutwa.

Lengo kuu la sekta ya makazi ni kuhakikisha watanzania wote wanakuwa na makazi bora. Ushiriki wa sekta binafsi kwenye maendeleo na huduma za makazi utahimizwa. Sekta ya habari na utangazaji ina lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji habari, uchambuzi na usambazaji wa habari hizo

kupitia vyombo mbalimbali vya mawasiliano ikiwa ni pamoja na magazeti, redio na televisheni. Ili kuboresha ustawi wa jamii, mazingira mazuri yatakayoruhusu ushiriki wa sekta binafsi na taasisi zisizo za kiserikali yatawekwa. Wanawake watapunguziwa mzigo wa kazi kwa kuhimiza uanzishwaji na usambazaji wa teknolojia inayofaa, na kuwaongezea jamii teknolojia mahiri. Uhamasishaji wa umma katika kuendeleza utamaduni wa taifa utakuzwa.

Mchango wa ufugaji nyuki katika mfumo wa kijamii unaonekana katika maeneo ya kuzalisha asali ambayo ni chakula na dawa, kuboresha uhifadhi wa mazingira kwa kuchavusha, na kuwaingizia watu kipato kwa kuuza asali, nta na huduma za kuchavusha. Mapato yanayotokana na ufugaji nyuki yanaweza kutumika kwa kulipia huduma za jamii kama vile elimu, afya, usafiri na kadhalika.

## 2. MATATIZO MAKUBWA YALIYOPO KISEKTA NA FURSA ZILIZOPO

Sekta ya ufugaji nyuki ina majukumu ya kusimamia rasilimali za nyuki na mimea ya chakula chao kwa misingi endelevu. Kipaumbele cha jumla na matatizo katika sekta hii vinatokana na masuala yafuatayo:

### *2.1 Usimamizi wa Rasilimali za Nyuki na Mimea ya chakula chao kwa ajili ya maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii na uboreshaji wa Mazingira.*

#### 2.1.1 Uwezo uliopo wa kuzalisha mazao ya Nyuki

Inakadiriwa kuwa uzalishaji wa mazao ya nyuki nchini Tanzania unaweza kufikia takriban tani 138,000 za asali na tani 9,200 za nta kwa mwaka kutokana na idadi ya makundi ya nyuki yanayokadiriwa kuwa milioni 9.2. Inakadiriwa kuwa kwa sasa ni tani 4,860 tu za asali na 324 za nta huzalishwa kwa mwaka. Hii ni asilimia 3.5 tu ya uwezo uliopo.

#### 2.1.2. Mchango wa Ufugaji Nyuki Katika Maendeleo ya Kijamii, Kiuchumi na Uhifadhi wa Mazingira

Sekta ya ufugaji nyuki inatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi na uhifadhi wa mazingira. Ufugaji nyuki ni chanzo cha chakula (asali, chavua, na majana ya nyuki), malighafi kwa ajili ya viwanda mbalimbali (mishumaa ya nta, vipodozi, nguo, mafuta ya kulainishia, na kadhalika), madawa na mapato kwa wafugaji wa nyuki. Inakadiriwa kuwa ufugaji nyuki unaingiza wastani wa dola za Kimarekani milioni 1.2 kwa mwaka katika

uchumi kutokana na mauzo ya asali na nta nje ya nchi. Vilevile, nyuki wanachavusha mimea mbalimbali.

### 2.1.3 Ufugaji Nyuki huboresha uhifadhi wa Bioanuwai

Ufugaji nyuki ambao ni stadi na sayansi ya utunzaji wa nyuki wa asali unatoa mchango mkubwa katika kuboresha bionuwai.

Nyuki wa asali hujumuisha wale waumao (Apis *mellifera spp.)* na wale wasiouma (Trigoma au *Melipona spp.).* Kupungua na kutoweka kwa nyuki wa asali kunaweza kutumika kama kiashirio cha kuharibika kwa mazingira.

## *2.2 Matatizo Yanayokwamisha Maendeleo ya Sekta ya Ufugaji Nyuki*

Matatizo makubwa yanayoikabili Sekta ya Ufugaji Nyuki ni:

### 2.2.1 Kutokuwapo kwa Sera na Sheria za Ufugaji Nyuki.

Tangu mwaka 1949 ilipoanzishwa rasmi kama Idara kwenye Kilimo, Sekta ya Ufugaji Nyuki nchini imeendeshwa kwa kupitia maelekezo na maagizo ambayo malengo yake yalikuwa:

(i) Kuboresha ufugaji wa nyuki kwa kuanzisha mizinga ya masanduku.

(ii) Kuongeza uzalishaji wa asali na nta.

(iii) Kuongeza mapato ya fedha za kigeni kwa kuuza asali na nta nchi za nje.

Zifuatazo ni baadhi ya sababu zinazoelezea umuhimu wa kuwa na Sera na sheria za ufugaji nyuki:

(iv) Kuna ushindani mkubwa wa ubora wa asali na nta katika masoko ya kimataifa. Katika ushindani huo, Mwaka 1991 huko Uingereza, asali ya Tanzania ilishinda kwa asilimia 100 ya ubora wa asali mahuluku. Udhibiti wa viwango vya ubora wa asali kutokana na vigezo vya 'HMF', rangi, ladha, mnato (viscosity), harufu nzuri na kadhalika, unahitaji maelekezo ya kisheria ambayo itabidi yafuatwe na watu wote wanaoshughulikia asali kabla ya kuwafikia walaji. Maelekezo hayo ya kisheria yanahitaji kuwa na lengo na mtazamo ulio wazi na unaoeleweka wa ufugaji nyuki kuhusu maendeleo na udhibiti wa viwango vya ubora wa asali.

(v) Katika miaka ya hivi karibuni, kuna wageni wengi hasa wanaotoka nchi za mashariki ya kati ambao wameonyesha nia ya kununua nyuki hai wa asali kutoka Tanzania. Nyuki wa asali wanaotoka nchi nyingine wameonekana kuwa na magonjwa mengi, vimelea na utitiri/nyenyere. Hivyo, ni lazima kuwe na sheria za kudhibiti uingizaji na usafirishaji nje nyuki wa asali. Sheria hizo hazina budi zijengwe katika misingi thabiti ya Sera ya Ufugaji Nyuki.

(vi) Hivi karibuni, wageni na wenyeji wameonyesha shauku ya kuwekeza katika shughuli za ufugaji nyuki. Hivyo basi Sera ya ufugaji nyuki inahitajika. Sera hii inatakiwa iwe wazi katika kutoa miongozo kwa wawekezaji wa ndani na nje kuhusu maeneo ya kuwekeza na motisha ambavyo vitapelekea uwekezaji na maendeleo endelevu.

Mabadiliko haya na mengine ya hivi karibuni ya kijamii na kiuchumi, pamoja na uzingatiaji zaidi wa uhifadhi wa mazingira kwa ajili ya kuleta maendeleo endelevu ya shughuli za Ufugaji Nyuki, yalipelekea kuundwa kwa Sera ya Ufugaji Nyuki (Rasimu ya 1993). Rasimu hii ilizangitia nafasi ya ushirikiano na uratibu miongoni mwa sekta mtambuka ambayo ingehimiza uhifadhi wa mazingira kwa kutekeleza miradi kama vile ya Ufugaji Nyuki-Kilimo Misitu na huduma za ugani - miradi ambayo inawaruhusu wafugaji nyuki kufuga nyuki katika Misitu ya Hifadhi, Mapori ya Akiba, kuendeleza teknolojia ya jadi ya ufugaji nyuki inayofaa na kupendwa na wafugaji wa nyuki na isiyoharibu mazingira. Pamoja na kutokuwapo kwa Sera rasmi ya Ufugaji Nyuki, uuzaji wa nta nje ya nchi umesimamiwa kisheria chini ya Kifungu cha 10 cha "Sheria za Uuzaji wa Mazao (Nta) Nje ya Nchi, ya 1957, Sura 137".

### 2.2.2 Kukosekana kwa Uratibu Rasmi wa masuala ya Sekta ya Ufugaji Nyuki kati ya Sekta hiyo na Sekta zinazohusiana za Misitu, Kilimo na Wanyamapori

Maendeleo yafuatayo ya kijamii, kiuchumi na kimazingira yamepelekea kuundwa kwa Sera ya Ufugaji Nyuki yenye lengo kuu la kuboresha uhifadhi wa nyuki wa asali na mazingira yake ili Taifa liendelee kunufaika na uhusiano wa kutegemeana kati ya nyuki wa asali na mimea.

(i) Mahitaji ya watu ya kufanya shughuli za ufugaji nyuki katika maeneo yaliyopo
karibu na misitu ya hifadhi na mapori ya akiba yameongezeka kwa kiasi kikubwa katika miaka ya hivi karibuni. Kwa mfano, katika Kikao cha Bunge la Bajeti cha mwaka 1996/97, zaidi ya maswali manne yaliulizwa na wafugaji nyuki kupitia wabunge wao,

wakiomba vibali vya kufuga nyuki katika sehemu za hifadhi. Ombi la aina hii linahitaji utaratibu wa utekelezaji wa Sera za Misitu, Wanyamapori na Ufugaji Nyuki.

(ii) Baada ya kukabiliwa na uhaba wa mimea ya chakula cha nyuki (hasa misitu ya miombo) unaosababishwa na ufyekaji wa misitu kwa ajili ya kilimo, uvunaji wa magogo na uchomaji wa mkaa, wafugaji wa nyuki wameomba watengewe sehemu maalumu kwa ajili ya ufugaji nyuki. Kwa mfano Wilaya ya Chunya waliomba hivyo. Hivyo basi, kunahitajika sera itakayohimiza uratibu na sekta za misitu na kilimo katika uanzishwaji na uendelezaji wa hifadhi za nyuki.

(iii) Katika miaka ya karibuni, juhudi za kuendeleza Ufugaji Nyuki-Kilimo Misitu ziliongezeka sana. Mojawapo ya sababu kuu za kutumia ardhi kwa Ufugaji Nyuki-Kilimo Misitu ni kuongeza uzalishaji wa mazao na huduma na wakati huo huo kuboresha uhifadhi wa mazingira. Sera inayohimiza maendeleo ya Mifumo ya Ufugaji Nyuki-Kilimo Misitu na mipango rasmi ya ushirikiano na uratibu miongoni mwa sekta mtambuka kwa ajili ya usimamizi endelevu wa mtindo huo haikwepeki.

(iv) Katika miaka ya karibuni utafiti umeonyesha kuwa kuendelea kuwapo kwa nyuki wa asali ambao ni maarufu kwa kuzalisha asali yenye ubora wa kiwango cha juu na ambayo inatumika kama dawa na ni muhimu kiuchumi, unatishiwa na sumu zitokanazo na viuwadudu, kufyeka mimea kwa ajili ya maendelelo ya kilimo na viwanda, na mioto ya kiholela inayowaua nyuki wa asali, kuharibu mimea ya chakula chao na makazi yao. Hatari hiyo ya kutoweka kwa nyuki wa asali imeongezeka kutokana na kutokuwapo kwa sheria inayowalinda. Baadhi ya wafugaji nyuki wa wilaya za Iringa na Njombe waliohojiwa mwaka 1992 walidai kuwa karibu miaka ishirini hadi thelathini iliyopita nyuki wasiouma walikuwapo kwa wingi katika maeneo ya vijiji vyao, na kwamba siku hizi hakuna kundi hata moja la nyuki hao. Pamoja na kuzalisha asali yenye ubora wa hali ya juu, nyuki wasiouma ni wachavushaji wazuri wa maua kutokana na miili yao midogo ukilinganisha na ile ya nyuki wa asali waumao. Vilevile, nyuki wasiouma wanafaa kuchavusha mazao ambayo hulimwa katika sehemu za makazi ya watu. Sera inayohimiza kuhifadhi na kuendeleza nyuki wa asali waumao na wasiouma kwa ajili ya uzalishaji wa mazao yatokanayo na nyuki hao, na pia kwa ajili ya huduma za uchavushaji inahitajika sana.

(v) Utafiti umeonesha kwamba nyuki wengi wa asali wanakufa katika mashamba ya kilimo kutokana na sumu ya viuwadudu. Aidha, baadhi ya wakulima wenye mwamko wameanza kukodi makundi ya nyuki wa asali kutoka kwa wafugaji nyuki kwa ajili ya kuchavusha mazao yao ya kilimo. Miongozo ya kisheria inahitajika si tu kulinda maslahi ya mkulima na ya mfugaji nyuki, bali pia maisha ya makundi ya nyuki wa asali ambao hutoa huduma za uchavushaji. Sera inayohimiza na kuelekeza matumizi endelevu ya nyuki wa asali kwa ajili ya uchavushaji inahitajika.

### 2.2.3 Kukosekana kwa Huduma Madhubuti za Ugani wa Ufugaji Nyuki

Huduma za ugani wa ufugaji nyuki haziwafikii ipasavyo wafugaji, watu wanaojihusisha na uchakataji wa mazao ya nyuki, watengenezaji wa vifaa vinavyotumika kufugia nyuki na wafanya biashara ya mazao ya nyuki. Matokeo yake ni kwamba bidhaa na huduma za sekta ya ufugaji nyuki bado ni za kiwango cha chini kwa aina na idadi; idadi ya wafugaji bado ni ndogo, na hivyo uzalishaji kitaifa wa mazao ya nyuki ni chini ya asilimia 5 ya uwezo uliopo. Takriban asilimia 90 ya shughuli za ufugaji nyuki hufanywa na wanaume wazee wakati ushiriki wa wanawake na vijana ni mdogo au haupo kabisa katika baadhi ya sehemu hapa nchini. Hali hii inatokana na imani potofu kwamba ufugaji nyuki ni kazi ya wanaume wazee, na unahusisha uchawi. Sababu nyingine ya wanawake na vijana kutokujihusisha kikamilifu katika ufugaji nyuki ni tabia ya nyuki wa asali kuuma, pamoja na kukosekana kwa ufahamu wa matumizi ya vifaa vya kinga. Vile vile, mbinu za usimamizi wa nyuki wa asali wasiouma hazijulikani kwa makundi hayo. Tatizo lingine kubwa linalohusiana na kutokuwapo kwa huduma madhubuti za ugani wa ufugaji nyuki, ni kukosekana kwa mwamko wa kutosha wa wanajamii kuhusu viwanda vinavyojikita kwenye mazao ya nyuki, viwanda ambavyo vingeweza kuajiri watu wengi na kuboresha maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

### 2.2.4 Ukosefu wa Takwimu za kutosha za kuwezesha kupanga Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Ufugaji Nyuki

Umuhimu wa takwimu kwa ajili ya kuleta maendeleo ya sekta hii uko katika kuwavutia na kuwapa imani wawekezaji na kuelekeza utayarishaji wa programu na miradi inayoweza kuwafanya watoe mikopo kwa wafugaji nyuki, watu wanaojihusisha na uchakataji wa mazao ya nyuki, watengenezaji wa vifaa vya kufugia nyuki na wafanyabiashara. Taarifa kuhusu rasilimali za nyuki na mimea ya chakula chao ambazo zipo katika kanda mbalimbali za kiikolojia nchini hazipatikani kwa urahisi. Taarifa nyingine muhimu za kusaidia utayarishaji wa mipango na utendaji kazi ni pamoja na:

- Uzalishaji wa mazao ya nyuki kwa kila kundi, majira ya mwaka na aina ya mzinga;
- Bei ya mazao ya nyuki kwenye soko la ndani na nje ya nchi;
- Bei za vifaa vya ufugaji nyuki;
- Uzalishaji kitaifa wa mazao ya nyuki na kiasi kinachouzwa nje ya nchi;
- Pato la Taifa.

### 2.2.5 Ukosefu wa Vifaa vya Kutosha na vinavyofaa kuchakatia na Kuhifadhia Mazao ya nyuki

Tatizo hili linapunguza ubora na wingi wa asali inayomfikia mlaji.

### 2.2.6 Ukosefu wa Huduma za Usafirishaji kwa ajili ya shughuli za Ugani na Mazao ya Nyuki

Tatizo hili linapunguza ushiriki wa wanawake na vijana katika ufugaji nyuki, usambazaji mazao na huduma.

### 2.2.7 Kukosekana kwa masoko ya kuaminika ya Mazao ya Nyuki

Taarifa zilizopo zinaonyesha kwamba huko Wilayani kuna asali na nta nyingi ambayo haina soko. Hali hii inawakatisha tamaa wafugaji nyuki pamoja na wale ambao wangependa kujiunga na shughuli hii.

## 3. LENGO NA MADHUMUNI YA SEKTA YA UFUGAJI NYUKI

**Lengo la jumla** la Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ni kuongeza mchango wa sekta hii kwa maendeleo endelevu ya Tanzania, na kuboresha uhifadhi na usimamizi wa maliasili yake kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

**Malengo ya kisekta** yanatokana na sera kuu za nchi pamoja na matatizo na nafasi ya kisekta katika ufugaji nyuki. Madhumuni ya sekta ya ufugaji nyuki ni kama yafuatayo:

- Kuhakikisha kuwapo kwa nyuki wa asali kwa kuwa na hifadhi za nyuki za kutosha na kuzisimamia kikamilifu;
- Kuongeza ubora na wingi wa asali, nta na mazao mengine ya nyuki na kuhakikisha upatikanaji wake katika misingi endelevu;
- Kuchangia katika kupunguza umaskini nchini;
- Kuboresha bioanuwai, kuongeza ajira na pato la fedha za kigeni,

kutokana na maendeleo ya viwanda na biashara ya mazao ya nyuki;
- Kuhakikisha udhibiti wa mifumo ikolojia kwa kutumia usimamizi wa pamoja wa wadudu waharibifu wa mazao na ukadiriaji wa athari kwa mazingira kabla ya uwekezaji ndani au kuzunguka hifadhi za nyuki na manzuki.
- Kuongeza uwezo wa kitaifa wa kusimamia na kuendeleza sekta ya ufugaji nyuki kwa kushirikiana na washikadau wengine.

Kutokana na madhumuni haya, **maeneo sita ya sera** yameainishwa, nayo ni:

- Kuanzisha hifadhi za nyuki na kuzisimamia kwa misingi endelevu;
- Kusimamia manzuki;
- Viwanda vinavyojikita katika ufugaji na mazao;
- Ufugaji nyuki katika maeneo ya Sekta mtambuka;
- Ufugaji nyuki kwa uhifadhi na usimamizi wa mifumo ikolojia;
- Taasisi na nguvukazi.

Katika kila moja ya maeneo haya ya sera, masuala muhimu ya kisera yanajadiliwa, matamko ya sera yanatolewa na nyenzo na maelekezo ya kufuatwa vimeelezwa.

# 4. MATAMKO YA SERA

## *4.1 Uanzishaji na Usimamizi endelevu wa Hifadhi za Nyuki*

**MADHUMUNI: Kuhakikisha kuwapo kwa nyuki wa asali kwa kuanzisha hifadhi za nyuki za kutosha na kuzisimamia kikamilifu**

### 4. 1. I Hifadhi za Nyuki za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa

Taarifa zilizopo zinaonyesha kwamba baadhi ya aina adimu za nyuki waumao na wasiouma zinatoweka katika maeneo mengi nchini. Hii inatokana na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli kama vile matumizi yasiyodhibitiwa ya viuwadudu, kufyekwa kwa misitu kwa ajili ya kilimo, upanuzi wa viwanda na uchomaji moto mapori. Uanzishwaji na usimamizi wa hifadhi za nyuki unaofanywa na serikali kuu na za mitaa au taasisi za utekelezaji, utahakikisha kuwapo kwa nyuki wa asali na rasilimali nyinginezo za ufugaji nyuki. Mifumo ya usimamizi wa pamoja wa hifadhi za nyuki itahimizwa. Makusudi ya kuwa na hifadhi za namna hii ni kama yafuatayo:

(a) Zitakuwa vitovu vya jene ya nyuki;
(b) Zitakuwa ni vyanzo vya makundi ya nyuki waumao na wasiouma;

(c) Zitaendeleza uhifadhi wa bioanuwai ya nyuki wa asali;
(d) Zitazalisha mazao ya nyuki.

***Tamko la Sera (1): Ili kuhakikisha kuwapo nyuki wa asali, serikali itaanzisha na kusimamia kwa misingi endelevu Hifadhi za Nyuki. Serikali au Taasisi za Utekelezaji zitaingia mikataba ya usimamizi wa pamoja na jumuiya za wananchi au vyama vingine vya watu wanaoishi kandokando ya Hifadhi za Nyuki. Ili kuhakikisha usimamizi endelevu wa Hifadhi za Nyuki mikataba hii itabainisha haki za watumiaji na mafao kwa wahusika kutoka katika hifadhi hizo.***

### 4.1.2 Hifadhi za Nyuki za Watu Binafsi

Uhifadhi wa wanyama na mimea unaofanywa na serikali kwa kupitia kwa mfano mapori ya akiba na misitu ya hifadhi, kumepelekea baadhi ya watu kuamini kuwa uhifadhi wa maliasili ni jukumu la serikali pekee. Aidha, wanaamini kwamba maliasili ni mali ya serikali tu, na kwamba watu binafsi hawana haki ya kuhifadhi, kusimamia, wala kutumia maliasili hizo kukidhi mahitaji yao ya kijamii na kiuchumi na kwamba kuna urasimu wa kupata leseni na vibali kwa ajili ya kutumia maliasili hizi.

Hata hivyo kuna baadhi ya makabila yanayotenga miti na misitu kwa ajili ya shughuli kama vile za kufuga nyuki, kufanya ibada, kupata maji, dawa, n.k. Uzoefu umeonyesha kuwa uhifadhi unaoshirikisha jumuiya unafaa na ni endelevu. Taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa wafugaji nyuki katika maeneo muhimu ya ufugaji ambao hukumbana na uhaba wa mimea ya chakula cha nyuki na makundi ya nyuki kutokana na kufyeka misitu kwa ajili ya kilimo, uvunaji wa magogo na uchomaji mkaa, wanaomba Hifadhi za Nyuki zianzishwe. Ushiriki wa washikadau katika kuhifadhi na kusimamia nyuki wa asali na rasilimali nyinginezo za nyuki kwa kushirikisha wananchi utahimizwa.

***Tamko la Sera (2): Ili kuwezesha ushiriki wa washikadau wote katika kuhifadhi na kusimamia nyuki wa asali, wafugaji nyuki binafsi na jumuiya mbali mbali watahimizwa kuanzisha, kusimamia na kumiliki Hifadhi za Nyuki kwa qjili ya ufugaji nyuki endelevu. Miongozo ya kuanzisha, kusimamia na kumiliki hifadhi hizo itasimamiwa na serikali.***

### *4.2 Usimamizi wa Manzuki*

**LENGO: Kuongeza ubora na wingi wa asali na nta na kuongeza mahitaji ya mazao hayo**

#### 4.2.1 Manzuki za Serikali

Kwa sasa, serikali inamiliki Manzuki zilizoko Handeni, Kondoa, Manyoni, na Kibondo. Manzuki hizo ni kwa ajili ya kufundishia na kufanyia utafiti wa ufugaji nyuki bora. Manzuki hizi zinakabiliwa na tatizo la ufinyu wa bajeti unaosababisha upungufu wa vitendea kazi na shida ya usafiri.

| |
|---|
| ***Tamko la Sera (3): Manzuki za Serikali (Handeni, Kondoa, Manyoni na_Kibondo) zitabinafsishwa.*** |

| |
|---|
| ***Tamko la Sera (4): Ili kuimarisha na kuendeleza huduma za ugani, serikali kuu na serikali za mitaa zitahamasisha taasisi za utekelezaji, mashirika yasiyo ya kiserikali na watu binqfsi kuanzisha manzuki za mifano ya ufugaji nyuki bora. Manzuki hizi zitasimamiwa kwa kufuata mipango iliyoidhinishwa, na zitatakiwa zijiendeshe zenyewe kifedha na kwa faida.*** |

#### 4.2.2 Manzuki za Binafsi

Inakadiriwa kuwa Tanzania inaweza kuzalisha tani 138,000 za asali na tani 9,200 za nta kwa mwaka, kiwango ambacho hakijafikiwa kwa sasa. Taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa ni tani 4,860 tu za asali na tani 324 za nta zinazozalishwa kwa mwaka. Uzalishaji huu ambao ni takriban asilimia 3.5 ya uwezo uliopo unafanywa na wafugaji binafsi na makundi madogo ya wafugaji. Uzalishaji wa asali unategemea ukubwa wa mizinga, upatikanaji wa mimea ya chakula cha nyuki na utunzaji mzuri wa manzuki. Taarifa zilizopo za uzalishaji kitaifa ni wastani wa kilo 15 za asali na kilo 1 ya nta kwa kundi la nyuki kwa mwaka. Katika sehemu ambazo asali huvunwa kwa zaidi ya msimu mmoja kwa mwaka, uzalishaji ni mkubwa.

Manzuki za binafsi zilizopo zina sifa zifuatazo:

- Zimeanzishwa na zinaendeshwa na wanaume wazee;
- Ziko mbali na vijiji, hivyo wafugaji nyuki wanakabiliwa na tatizo la usafiri;
- Mizinga imetundikwa katika miti mirefu ili kuepuka moto, wanyama, wadudu waharibifu na mafuriko;
- Uvunaji wa asali hufanyika usiku, hivyo wafugaji nyuki wanakabiliwa na hatari ya kuvamiwa na wanyama wakali-,

- Wafugaji nyuki hawatumii mavazi ya kinga wakati wa kurina hivyo huumwa na nyuki.
- Kutokana na haya, wafugaji nyuki wanakabiliwa na hatari ya kuvamiwa na wanyama wakali na hata kuumwa na nyuki wakali. Vile vile, wafugaji hao wanakabiliwa na tatizo la usafiri kutoka katika sehemu za ufugaji mpaka kwenye viwanda vya asali na nta.

Sababu hizo ndizo ambazo zimewafanya wanawake na vijana wauone ufugaji nyuki kuwa ni shughuli ya kiuchumi isiyovutia. Hali hii huwakatisha tamaa wawekezaji wapya katika ufugaji nyuki, hivyo kusababisha uzalishaji mdogo.

***Tamko la Sera (5): Ili kuhakikisha kuna upatikanaji endelevu wa mazao ya nyuki na huduma bora za uchavushaji, uanzishwaji na usimamizi wa Manzuki za kibinafsi vitahimizwa.***

**Tamko la *Sera (6): Ili kuhakikisha kuwapo kwa* usimamizi mzuri *wa rasilimaii* za nyuki *wa asali* na mimea ya chakula *chao kwa* ajili ya *uzalishaji endelevu wa* mazao ya nyuki, *sekta binafsi* itahimizwa kuanzisha na kusimamia ufugaji nyuki katika mfumo wa kilimo-misitu.**

***Tamko la Sera (7): Ili kuwavutia wanawake na vijana washiriki kikamilifu katika ufugaji nyuki, huduma mahsusi za ugani kwa ajili ya makundi haya zitaanzishwa.***

## *4.3 Viwanda vinavyojikita kwenye shughuli za Ufugaji Nyuki na Mazao ya Nyuki*

**LENGO: Kukuza mchango wa ufugaji nyuki kwa maendeleo na kupunguza umasikini**

### 4.3.1 Vifaa vya Ufugaji Nyuki

Viwanda vinavyojikita katika ufugaji nyuki na mazao yatokanayo na nyuki, huhusisha utengenezaji wa vifaa vya ufugaji nyuki ambavyo ni mizinga, mavazi ya kinga, mabomba ya moshi, patasi ya mzinga, vifaa vya kuhifadhia asali na nta, mashine ya kukamulia asali, vifaa vya kuchujia asali na nta n.k. Matatizo makubwa yanayovikabili viwanda vinavyojikita katika ufugaji nyuki yanajumuisha:

- Jamii kutofahamu kuwapo kwa viwanda mbalimbali vinavyojikita kwenye shughuli hii;
- Ukosefu wa maarifa na ujuzi wa namna ya kutengeneza biadhaa

mbalimbali kutokana na mazao ya nyuki;
- Ukosefu wa mtaji na malighafi za kuzalishia bidhaa;
- Udhaifu katika usimamizi wa rasilimali za kutengenezea mizinga.

Udhaifu katika usimamizi wa rasilimali za kutengenezea mizinga kwa kutumia magome na magogo umesababisha uharibifu wa miti. Suluhisho mojawapo la tatizo hili ni kuanzishwa kwa mkabala timilifu unaohusisha watumiaji mbalimbali wa jamii ya miti itoayo magome na magogo ya kutengenezea mizinga ya nyuki ili waweze kutumia mti huo huo kwa ajili ya mbao, mkaa, kuni au kuchomwa ili kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo. Magome yake lazima yatumike kutengenezea mizinga kwanza kabla ya kutumiwa kwa shughuli nyingine. Mamlaka ya mfumo wa uratibu unaohusisha sekta mtambuka itaanzishwa ili kuboresha utengenezaji wa vifaa sahihi vya ufugaji nyuki.

**Tamko la *Sera (8): Upatikanaji wa vifaa sahihi vya Ufugaji Nyuki utahakikishwa kwa kuhimiza Taasisi za* Utekelezaji, *mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta binafsi, wafanye* utafiti *wa* maendeleo ya *vifaa hivi* na kusambaza *vifaa* na matokeo ya utafiti huo *kwa Wafugaji Nyuki.***

**Tamko la *Sera (9): Ili kuwavutia wawekezaji katika uzalishaji wa vifaa vya ufugaji* nyuki, utoaji *wa* mikopo *utahimizwa. .***

***Tamko la Sera (10): Ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali, matumizi mbalimbali ya miti inayofaa kutengenezea mizinga yataratibiwa. Malighafi mbadala ya kutengenezea mizinga sahihi na ya bei nafuu itatafutwa kupitia utafiti. Mfumo rasmi wa uratibu kati ya mamlaka za ufugaji wa nyuki na misitu utaanzishwa.***

### 4.3.2 Viwanda na Bidhaa Zitokanazo na Asali

Viwanda na bidhaa zitokanazo na asali huhusisha matumizi ya asali kama kiambato muhimu katika viwanda vya madawa, uhifadhi wa chakula, kutengeneza wanzuki na aina nyingine za pombe. Matatizo makubwa yanayovikabili viwanda vya aina hii ni pamoja na:

- Kutokuwapo uhakika wa upatikanaji wa asali kutokana na mfumo mbaya wa masoko;
- Ukosefu wa mtaji au mikopo kwa ajili ya wawekezaji;
- Kukosekana kwa mwamko miongoni mwa wananchi kuhusu matumizi mbalimbali ya asali na bidhaa zake.

**Tamko la Sera (I1): Uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vinavyojikita kwenye asali na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na asali utahimizwa. Utafiti na maendeleo kuhusu matumizi mengineyo ya asali utakuzwa.**

### 4.3.3 Viwanda na Bidhaa zitokanazo na Nta

Viwanda na bidhaa za nta hujumuisha shughuli za biashara kama: utengenezaji wa mishumaa, matumizi ya nta kama kiambato muhimu katika madawa, vipodozi, mafuta ya kulainishia, polishi, chingamu, nguo, tetefya, karatasi n.k.

Viwanda hivi vinakabiliwa na matatizo makubwa yafuatayo:

- Kukosekana kwa taarifa kuhusu mbinu za uzalishaji zinazofaa;
- Kutokuwapo takwimu za kutosha ili kuhamasisha uwekezaji;
- Kutokuwapo uhakika wa upatikanaji wa nta.

***Tamko la Sera (12): Uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda na bidhaa zitokanazo na nta utahimizwa ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa bidhaa hizo kwa mahitaji ya ndani na nje ya nchi. Utafiti na maendeleo ya matumizi mengineyo ya nta na usambazaji wa matokeo ya utafiti huo kwa watumiaji vitahimizwa.***

### 4.3.4 Viwanda na Bidhaa zitokanazo na uchavushaji

Katika baadhi ya nchi zilizoendelea nyuki wanatumika sana katika kuchavusha mimea ya kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao. Nchini Tanzania ufugaji nyuki kwa ajili ya huduma ya uchavushaji haujaendelezwa. Hali hii inatokana na:-

- Kukosekana kwa miongozo ya kiufundi na misaada kwa wafugaji nyuki na wakulima kuhusu namna ya kuanzisha na kusimamia makundi kwa ajili ya uchavushaji;
- Kutokuwapo kwa uhakika wa kupatikana kwa makundi imara ya nyuki yanapohitajika;
- Kutokuwapo kwa ushirikiano rasmi na uratibu wa sekta za ufugaji nyuki na kilimo katika kupanga na kutekeleza programu na miradi

ya uchavushaji.

- Nyuki kwa ajili ya uchavushaji madhubuti wanaweza kupatikana kwa kuanzisha na kutekeleza uzalishaji wa makundi bora ya nyuki.

Uzoefu uliopo Marekani, Uholanzi, Kanada na Uingereza wa kutumia nyuki kwa shughuli za uchavushaji wa mazao ya kilimo utatumika ili kuwavutia wawekezaji.

***Tamko la Sera (13): Wakulima watahamasishwa kutumia nyuki katika uchavushaji wa mimea yao ili kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao.***

#### 4.3.5 Viwanda Vingine Vinavyotegemea Bidhaa za Nyuki

Kulingana na ripoti zilizopo, waganga wengi wa jadi nchini Tanzania wanatumia sumu ya nyuki, propolisi na mazao mengine ya nyuki katika kutibu magonjwa mbali mbali ya binadamu. Ingawa taarifa zilizopo zinaonyesha kwamba sumu ya nyuki inaweza kutibu magonjwa ya masikio, baridi yabisi na kupunguza hisia kali kama mtu akitumia kipimo kilichoshauriwa na daktari, bado hakuna matokeo ya utafiti yaliyothibitishwa kuhusu matumizi ya mazao hayo ya nyuki nchini.

Mazao mengine yanayohitaji kufanyiwa utafiti, kuendelezwa na kutafutiwa masoko ni:

- Feromoni za malikia ambazo viziduzi vyake vinaweza kutumika kutafiti na kuendeleza usimamizi. unganishi wa wadudu waharibifu;
- Majana ya nyuki kwa kutengenezea "supu ya nyuki" inayopendwa sana miongoni mwa makabila kadhaa nchini kama chakula chenye protini nyingi kitokanacho na nyuki wa asali;
- Maziwa ya nyuki kwa ajili ya kutengenezea madawa na vipodozi.

***Tamko la Sera (14): Ili kukuza matumizi ya mazao mengine ya nyuki, taasisi za utafiti, sekta binafsi na jumuiya kwa ujumla watahamasishwa ili wawekeze katika utafiti na uendelezaji wa mazao hayo.***

#### 4.3.6 Utalii wa Kiikolojia

Utalii wa kiikolojia katika hifadhi za nyuki na manzuki bado haujaanzishwa nchini. Pamoja na kwamba hakuna kumbukumbu zinazoonyesha kuwapo kwa utalii wa namna hiyo katika nchi nyingine, hatua za kuanzisha na kuendeleza utalii huu zinatarajiwa kuwa na matokeo mazuri kutokana na

kuwapo uwezekano mkubwa wa kufanyika hapa nchini. Sekta ya ufugaji nyuki itashirikiana na washikadau wengine wanaojihusisha na kuendeleza utalii ili kutayarisha vijitabu vya kuelekeza utalii kwenye hifadhi za nyuki na manzuki. Huduma na zana za nyuki kama mizinga ya maonesho, asali ya masega na nyuki wa kuuza, vitaendelezwa.

***Tamko la Sera (15): Sekta binafsi na jumuiya kwa jumla zitahimizwa kuendeleza na kutangaza utalii wa kiikolojia katika hifadhi za nyuki, manzuki na mazao yatokanayo na nyuki. Mfumo wa kisheria wa uratibu na sekta ya utalii utaanzishwa.***

### *4.4. Ufugaji Nyuki Katika Maeneo ya Sekta Mtambuka*

**LENGO:** **Kuboresha bioanuwai, kuongeza ajira na mapato ya fedha za kigeni kwa kuendeleza viwanda vinavyojikita kwenye mazao ya nyuki na biashara**

#### 4.4.1 Ufugaji Nyuki Katika Ardhi huria

Uwezo wa kuanzisha na kusimamia manzuki katika ardhi huria nchini bado ni mdogo. Utafutaji wa asali porini unasemekana kuhusika katika ardhi huria. Wafugaji nyuki wanasita kuanzisha manzuki katika ardhi huria kutokana na sababu zifuatazo:

- Kuenea kwa wizi wa mazao ya nyuki na mizinga;
- Makundi ya nyuki kuharibiwa na moto na nyegere;
- Ukosefu wa fedha za kuanzishia miradi na mavazi ya kinga;
- Baadhi ya maeneo kutokuwa na mimea ya kutosha ya chakula cha nyuki na kuyafanya makundi ya nyuki yahame. Hali hii inaweza kurekebishwa kwa kupanda mimea ya chakula cha nyuki.

Mikakati mingine ya kuboresha mazingira kwa ajili ya ufugaji nyuki katika ardhi huria ni pamoja na kutumia bomba la moshi na mavazi ya kinga ili kuzuia uchomaji moto maeneo hayo, kudhibiti wizi wa makundi ya nyuki, kuzuia nyegere na kupata hatimiliki ya manzuki.

***Tamko la Sera (16): Mfugaji nyuki mmoja mmoja, vikundi na vyama vya ushirika vya wafugaji nyuki vitahamasishwa kuanzisha na kusimamia manzuki katika ardhi huria. Ili kuhakikisha kwamba kuna usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali ya nyuki na chakula chao, vifaa vya ufugaji nyuki na usimamizi sahihi vitatumika.***

### 4.4.2 Ufugaji Nyuki Katika Maeneo ya Kilimo

Usimamizi wa manzuki katika maeneo ya kilimo unafanywa kwa kiasi kidogo kwa mfano, katika mashamba ya kahawa ambapo, ni kawaida kuona mizinga ya nyuki iliyotundikwa juu ya miti mirefu ili wapita njia, wanyama wafugwao na wakulima wasiumwe na nyuki. Hatua nyingine za usalama zinajumuisha kutengeneza uzio wa miti kuzunguka sehemu ya manzuki au kuweka manzuki mbali na maeneo waliko watu. Wakulima au wafugaji nyuki hawaanzishi manzuki katika au karibu na maeneo yao ya kilimo kwa sababu wanaogopa kuumwa na nyuki. Hata hivyo, baadhi ya wakulima wameanzisha manzuki za nyuki wasiouma katika makazi yao ambazo huwahakikishia upatikanaji wa asali na huduma za uchavushaji wa mazao yao ya kilimo.

Sababu nyingine za kutoanzishwa kwa manzuki ndani ya au kandokando mwa maeneo ya kilimo ni:

- Wafugaji nyuki wanahofia kupoteza makundi yao ya nyuki kutokana na sumu za viuwadudu;
- Kampeni za kueneza asali mahuluku kama kigezo muhimu cha ubora kinawafanya wafugaji nyuki waanzishe manzuki mbali na mashamba ili kuepuka uchafuzi wa asali kutokana na viuwadudu.

Tatizo la sumu itokanayo na viuwadudu linaweza kutatuliwa kwa kuwa na makubaliano ya usimamizi wa suala la viuwadudu waharibifu kati ya wafugaji nyuki na watumiaji viuwadudu.

| |
|---|
| ***Tamko la Sera (17): Uanzishwaji na usimamizi wa manzuki katika maeneo ya kilimo utahimizwa ili kuboresha uzalishaji wa mazao ya nyuki na huduma za uchavushaji. Huduma za uchavushaji zitaboresha mazao ya kilimo.*** |

### 4.4.3 Ufugaji Nyuki Katika Mapori ya Akiba

Hivi karibuni ufugaji nyuki katika baadhi ya Mapori ya Akiba umeruhusiwa chini ya mikataba maalum baina ya uongozi wa mapori hayo na wafugaji nyuki. Hatua hii ni mkakati wa kuwashirikisha wananchi katika uhifadhi endelevu wa maliasili.

Pamoja na mambo mengine makubaliano maalum kati ya uongozi wa mapori ya akiba na wafugaji nyuki yanajumuisha:

- Wafugaji nyuki washiriki katika kuhifadhi rasilimali ya wanyamapori kwa kutoa habari kuhusu kuwapo majangili na mahali walipo na wao wenyewe kutokushiriki katika ujangili;
- Wafugaji nyuki watumie bomba la moshi wakati wa kurina asali;
- Kalenda ya shughuli za ufugaji nyuki ijulikane kwa uongozi wa pori husika ili iweze kufuatiliwa.

**Tamko la *sera (18): Uanzishwaji* na usimamizi *wa* manzuki katika *mapori ya akiba utakaofanywa na Jumuiya, mfugaji nyuki mmoja mmoja, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za utekelezaji utahimizwa. Makubaliano ya usimamizi wa pamoja, yakijumuisha mgawanyo wa mafao yatafanywa kati ya serikali na wafugaji nyuki. Utaratibu rasmi wa ushirikiano kati ya mamlaka za Ufugaji Nyuki na Wanyamapori utaanzishwa ili kuboresha uratibu wa shughuli chini ya mipango ya usimamizi wa mapori ya akiba husika.***

### 4.4.4 Ufugaji Nyuki Katika Hifadhi za Taifa

Ufugaji wa nyuki katika Hifadhi za Taifa hauruhusiwi. Hata hivyo mahitaji ya jumuiya zilizoungana (kama vile ya Vyama vya Ushirika vya wafugaji nyuki) na mfugaji nyuki mmoja mmoja yanaongezeka na wangependa kufuga nyuki katika maeneo haya ambayo yana rasilimali nyingi kwa ajili za ufugaji nyuki. Rasilimali hizo ni pamoja na:

- Idadi kubwa ya makundi ya nyuki;
- Mimea ya chakula cha nyuki na maji; na
- Kuwapo kwa wafugaji nyuki wa jadi karibu na Hifadhi za Taifa.

Kuanzishwa kwa dhana mpya za uhifadhi, kama ushirikishwaji wa wananchi kutapelekea utawala wa Hifadhi za Taifa kupitia upya sheria za Wanyamapori ili ufugaji nyuki ambao hauharibu mazingira uruhusiwe kufanyika katika hifadhi hizo.

**Tamko la Sera (19): Uwezekano wa kufuga nyuki katika Hifadhi za Taifa utaangaliwa kwa kushirikiana na mamlaka zinazohusika na uhifadhi wa Wanyamapori.**

### 4.4.5 Ufugaji Nyuki Katika Misitu ya Hifadhi na Mashamba ya Miti

Usimamizi wa Manzuki katika Misitu ya Hifadhi na mashamba ya miti unafanyika kwa kiasi fulani kwa kufuata Sheria ya Misitu. Inategemewa kuwa kuanzishwa kwa dhana mpya ya usimamizi wa pamoja wa misitu, kutajumuisha vile vile usimamizi wa pamoja wa manzuki. Utaratibu huu utazingatia masilahi ya washikadau husika.

> ***Tamko la sera (20): Sekta binafsi na jumuiya zilizoungana zitahimizwa kuanzisha na kusimamia manzuki katika misitu ya hifadhi na mashamba ya miti. Manzuki hizo zitasimamiwa chini ya utaratibu wa usimamizi wa pamoja wa misitu ambao utazingatia masilahi ya washikadau. Utaratibu rasmi baina ya mamlaka za ufugaji nyuki na misitu utaanzishwa ili kufanikisha ufugaji nyuki katika misitu ya hifadhi na mashamba ya miti.***

## *4.5 Ufugaji Nyuki katika Kuhifadhi na Kusimamia Mifumo Ikolojia*

**LENGO:** **Kuhakikisha uthabiti wa mifumo ikolojia kwa kutumia usimamizi unganishi wa wadudu waharibifu na ukadiriaji wa athari kwa mazingira ndani na au kuzunguka Hifadhi za Nyuki na Manzuki**

### 4.5.1 Usimamizi wa Viuwadudu

Usimamizi wa viuwadudu hivi sasa umeachwa mikononi mwa watumiaji; na hakuna utaratibu wa sekta mtambuka wa kuhimiza usimamizi wa viuwadudu unaojumuisha washikadau mbalimbali ambao wanaathiriwa na viuwadudu. Tatizo mojawapo litokanalo na kutokuwapo kwa usimamizi unganishi wa matumizi ya viuwadudu ni kuwaua nyuki wa asali na wadudu wengine wenye manufaa. Wakati mwingine mabaki ya viuwadudu huonekana katika asali. Hii hupunguza ubora wa asali unaotakiwa wa zao la asali mahuluku unaohitajika sana katika soko. Hivyo, matumizi holela ya viuwadudu yanawafanya wafugaji nyuki kupoteza makundi ya nyuki na kukosa asali. Ili kuendeleza siyo tu maisha ya nyuki bali hata viwanda vya ufugaji nyuki, makubaliano kuhusu usimamizi unganishi wa wadudu waharibifu yatakuzwa. Makubaliano hayo, miongoni mwa mambo mengine yanaweza kujumuisha:

(a) Kutumia viuwadudu usiku wakati ambao nyuki hawatafuti chakula ;
(b) Kutumia viuwadudu vyenye athari hasi ndogo kwa nyuki;
(c) Kuepuka kutumia viuwadudu katika kipindi ambacho maua yanachavushwa na nyuki;
(d) Mfugaji nyuki kuwafungia nyuki wakati viuwadudu vinapotumika.

***Tamko la sera (21): Ili kuwalinda nyuki wasidhuriwe na viuwadudu, makubaliano ya usimamizi unganishi wa wadudu waharibifu baina ya watumiaji wa viuwadudu na wafugaji nyuki yataanzishwa. Utaratibu baina ya mamlaka za Ufugaji nyuki na taasisi nyingine zinazojihusisha na matumizi ya viuwadudu utaanzishwa. Inategemewa kuwa utaratibu huu utapunguza matumizi holela ya viuwadudu.***

### 4.5.2 Ukadiriaji wa Athari kwa Mazingira

Nyuki, mimea ya chakula chao na mazao katika hifadhi za nyuki na manzuki vinaweza kuharibika kutokana na shughuli za uchimbaji madini, ujenzi wa barabara, utumiaji wa viuwadudu, ufyekaji, mioto n.k. Hivyo basi, ili kuepuka uharibifu wa mazingira usio wa lazima ni budi ukadiriaji wa athari kwa mazingira ufanyike na utumike ili kuzuia madhara hayo. Nyuki ni wepesi kudhurika kutokana na uharibifu wa mazingira; hivyo wanaweza kutumika kama kiashirio katika ukadiriaji wa athari kwa mazingira.

***Tamko la Sera (22): Ukadiriaji wa athari kwa mazingira utahitajika kwa uwekezaji utakaoanzishwa ndani au kuzunguka hifadhi za nyuki na manzuki ili kuzuia uharibifu wa nyuki, mazao na mimea ya chakula chao.***

### *4.6 Asasi na Nguvukazi*

**MALENGO: Kukuza uwezo wa kusimamia na kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki kwa kushirikiana na washikadau**

### 4.6.1 Mfumo wa kupanga, kutekeleza na kuratibu shughuli za Ufugaji Nyuki

Uwezo wa kupanga, kutekeleza na kuratibu shughuli za ufugaji nyuki ni dhaifu kutokana na:

- Kutokuwapo kwa sera na sheria za ufugaji nyuki;
- Kutokuwapo kwa wataalamu wa masuala ya mipango na sera;

- Kutokuwapo kwa uratibu rasmi wa sekta husika kama vile za misitu, kilimo na wanyamapori;
- Kutokuwapo kwa mfumo wa kubadilishana maoni baina ya watoaji wa huduma za ugani na washikadau wengine katika maendeleo ya ufugaji nyuki;
- Upungufu wa takwimu za kusaidia kutayarisha mipango ya kuendeleza sekta ya ufugaji nyuki;
- Kutokuwapo kwa vifaa vya ukusanyaji na kuhifadhia data na habari nyingine za ufugaji nyuki.

***Tamko la Sera (23): Uwezo wa kuchambua Sera na kutayarisha mipango kwa ajili ya sekta ya ufugaji nyuki utaimarishwa. Mkazo utawekwa katika mipango kimkakati na uratibu.***

### 4.6.2 Mfumo wa Kisheria na Udhibiti

Sekta ya ufugaji nyuki imeendeshwa bila ya kuwa na sera na sheria rasmi tangu mwaka 1949 wakati ilipoanzishwa rasmi kama idara chini ya sekta ya kilimo. Maendeleo ya sekta ya ufugaji nyuki yalijikita kwenye maagizo na maelekezo ya kitaalamu na kiutawala. Pamoja na kutokuwapo kwa sera na sheria rasmi za ufugaji nyuki, uuzaji wa nta nje ya nchi umekuwa ukishughulikiwa kisheria chini ya kifungu cha 10 cha 'Sheria za Uuzaji wa Mazao (Nta) Nje ya Nchi, Mwaka wa 1957, Sura ya 137"

Kutokuwapo kwa sheria ya ufugaji nyuki kumepelekea matatizo yafuatayo ambayo yanakwamisha maendeleo ya sekta hii:

- Kutokuwapo kwa muafaka na sekta mtambuka kuhusu masuala ya sera na mengine yanayohusu uhifadhi endelevu wa nyuki na mazingira;

- Kutokuwapo kwa kanuni na taratibu za kutoza ushuru wa mazao ya nyuki na huduma zitolewazo na sekta vimeikosesha serikali mapato;
- Kutokuwapo kwa sheria za uingizaji na usafirishaji nje wa nyuki na mazao yake (isipokuwa nta) na vifaa vya ufugaji nyuki, kumepelekea udhaifu katika udhibiti wa waagizaji na wasafirishaji wa vitu hivyo;
- Kutokuwapo kwa vigezo na viashirio vya usimamizi endelevu wa rasilimali ya nyuki kumeleta ugumu katika kuandaa miongozo na mipango ya kusimamia ufugaji nyuki katika macneo mbalimbali yasiyohifadhiwa, hifadhi za nyuki, maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wanyamapori, misitu ya hifadhi na mashamba ya miti na maeneo ya kilimo.

Kuundwa na baadaye kurekebishwa kwa sheria ya ufugaji nyuki kutafuata sera iliyoidhinishwa kwa kuzingatia sheria za sekta nyingine husika. Vigezo na viashirio vya kitaifa kwa ajili ya usimamizi endelevu wa rasilimali za ufugaji nyuki vitaanzishwa. Miongozo ya usimamizi wa manzuki itatengenezwa kuzingatia vigezo na viashirio hivyo. Mipango ya usimamizi wa hifadhi za nyuki na manzuki katika maeneo yasiyohifadhiwa na yaliyohifadhiwa na maeneo ya kilimo itatayarishwa. Uwezo wa Idara ya Misitu na Nyuki katika kufuatilia utekelezaji wa mipango ya ufugaji nyuki utaimarishwa. Mirabaha na ada nyinginezo za mazao ya nyuki na huduma zitaanzishwa na kurekebishwa mara kwa mara ili kuakisi thamani yake ya kiuchumi. Mapato yatakusanywa kwa ufanisi. Bei za mazao ya nyuki, uchavushaji na huduma nyingine zitakazouzwa kutoka katika hifadhi za nyuki na manzuki za serikali kuu na serikali za mitaa zitapangwa kufuatana na thamani yake katika soko huria.

***Tamko la Sera (24): Sheria ya ufugaji nyuki itaundwa kwa kuzingatia sera mpya. Sheria itakuwa na ulinganifu na sheria za sekta nyingine husika na itafanyiwa marekebisho kila inapohitajika.***

***Tamko la Sera (25): Mirabaha na ada nyingine za mazao ya nyuki na huduma zitaanzishwa na kusimamiwa. Mirabaha na ada hizi zitarekebishwa mara kwa mara ili kuakisi thamani yake ya kiuchumi.***

***Tamko la Sera (26): Bei za mazao ya nyuki na huduma kutoka katika manzuki za binafsi na za serikali zitapangwa kulingana na thamani yake katika soko huria.***

***Tamko la sera (27): Uingizaji wa nyuki, mazao yake na vifaa vya ufugaji nyuki utadhibitiwa ili kuzuia magonjwa na vimelea kwa nyuki wa asali.***

***Tamko la sera (28): Uendelezaji na usimamizi wa nyuki wa asili vitapewa kipaumbele.***

***Tamko la Sera (29): Vigezo na viashirio vya kitaifa vya usimamizi endelevu wa rasilimali za ufugaji nyuki vitawekwa. Miongozo ya usimamizi wa manzuki katika maeneo mbalimbali kama vile mashamba, maeneo yaliyohifadhiwa na yasiyohifadhiwa itaandaliwa kwa kuzingatia vigezo na viashirio hivyo. Aidha, mipango ya usimamizi wa hifadhi za nyuki na manzuki itaandaliwa ipasavyo.***

### 4.6.3 Utawala katika Sekta ya Ufugaji Nyuki

Utawala wa ufugaji nyuki chini ya Idara ya Misitu na Nyuki, kama sekta nyingine za maliasili, uko chini ya mamlaka tatu ambazo ni Halmashauri za wilaya, Tawala za Mikoa, na Wizara ya Maliasili na Utalii. Afisa Nyuki wa Wilaya ambaye anasaidiwa na Maafisa Nyuki wa Tarafa, na Maafisa Nyuki wa Kata, anasimamia maendeleo ya sekta ya ufugaji nyuki katika wilaya.

Utoaji wa maamuzi kuhusu masuala ya ufugaji nyuki unaathiriwa na kutokuwapo kwa mfumo mzuri wa habari na data. Aidha, maslahi duni ya watumishi wa serikali na mazingira magumu ya kufanyia kazi vimekuwa vikipunguza ari ya utendaji kazi.

Uwezo wa Idara ya Misitu na Nyuki kutoa miongozo ya kiutawala na kiufundi kwa Mikoa na Wilaya kuhusu ufugaji nyuki unaathiriwa na upungufu wa watumishi na ufinyu wa bajeti.

Upungufu wa watumishi upo pia katika ngazi ya wilaya. Baadhi ya wilaya zenye uwezo mkubwa wa ufugaji nyuki hazina watumishi husika. Hali hii inapelekea uratibu wa sekta mtambuka kuhusu masuala ya sera na shughuli nyingine kuwa mgumu.

***Tamko la Sera (30): Utawala wa Sekta ya Ufugaji Nyuki utalenga katika kuendeleza sera, udhibiti, ufuatiliaji na uwezeshaji. Aidha, madaraka yatakasimiwa kwa mamlaka za Mikoa na Wilaya. Usambazaji na upashanaji wa habari pamoja na huduma za mafunzo ya kitaalam_vitaimarishwa.***

Utawala wa sekta ya ufugaji nyuki chini ya Idara ya Misitu na Nyuki utaendelezwa kwa kuzingatia marekebisho ya sekta ya umma. Uhusiano na uratibu wa masuala ya kitaalamu kati ya Idara na Mikoa/Wilaya utaimarishwa.

Wilaya zenye rasilimali kubwa ya nyuki zitahimizwa kuajiri watumishi na kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya uendelezaji wa sekta hii. Ili kuboresha utendaji, watumishi wataendelezwa kimafunzo.

Uwezo wa utawala wa sekta ya ufugaji nyuki katika kutoa taarifa za kisheria na ukadiriaji wa rasilimali na masoko kwa mikoa na wilaya na washikadau wengine utaimarishwa. Aidha, upashanaji wa habari baina ya sekta ya nyuki na washikadau wengine utaimarishwa.

#### 4.6.4 Serikali za Mitaa

Uwezo wa kiufundi wa serikali za mitaa katika shughuli za ufugaji nyuki ni mdogo. Wilaya nyingine hazijui kwamba zina utajiri wa rasilimali ya nyuki; na hivyo ufugaji nyuki haupewi kipaumbele katika mipango yake ya maendeleo. Usimamizi endelevu wa rasilimali ya nyuki katika ngazi ya wilaya unakabiliwa na matatizo yafuatayo:-

- Upungufu wa watumishi;
- Kutokuwapo kwa uratibu miongoni mwa sekta ya ufugaji nyuki na sekta za misitu, kilimo na wanyamapori kuhusu masuala ya ugani, ufugaji nyuki katika mapori ya akiba, misitu ya hifadhi, programu za uchavushaji wa mazao ya kilimo, na usimamizi unganishi wa wadudu waharibifu;
- Upungufu wa huduma za ugani.
- Upungufu wa takwimu za kusaidia kutayarisha mipango ya kuendeleza sekta ya ufugaji nyuki.

***Tamko la Sera (31): Uwezo wa serikali za mitaa katika kusimamia rasilimali ya nyuki utaimarishwa na mfumo wa uratibu kati ya serikali za mitaa na serikali kuu utaanzishwa na kuimarishwa.***

Ili kuhakikisha uhifadhi endelevu wa rasilimali ya nyuki, serikali za mitaa zitahimizwa kuajiri watumishi wa ufugaji nyuki wenye sifa zinazofaa.

#### 4.6.5 Utafiti wa Ufugaji Nyuki

Utafiti wa ufugaji nyuki umekuwa ukifanywa bila ya kuwa na mpango mkuu na vipaumbele vya utafiti havijawekwa wazi. Utekelezaji wa utafiti na maendeleo katika sekta ya ufugaji nyuki umekuwa ukikwamishwa na uhaba wa nguvukazi na ufinyu wa bajeti. Aidha, utafiti wa ufugaji nyuki haujaendana na mahitaji kutokana na uhusiano na mawasiliano hafifu kati ya asasi ya utafiti na washikadau.

***Tamko la Sera (32): Utafiti wa ufugaji nyuki kama msingi wa uendelezaji na usimamizi wa sekta ya ufugaji nyuki utakuzwa na kuimarishwa. Shughuli za utafiti zitagharimiwa kwa njia ya uchangiaji wa gharama na mifuko ya utafiti.***

***Tamko la Sera (33): Mfumo wa sheria kwa ajili ya ushirikiano na uratibu wa shughuli za utafiti kati ya Kituo cha Utafiti wa Ufugaji Nyuki Njiro (NBRC) na asasi nyingine husika za utaftti utaanzishwa. Ili kuimarisha shughuli za utafiti wa ufugaji nyuki nchini, uwezekano wa kukitenganisha kituo cha utafiti wa nyuki Njiro kutoka asasi ya utafiti wa wanyamapori Tanzania (TAWIRI) utaangaliwa.***

***Tamko la Sera (34): Vipaumbele vya utafiti wa ufugaji nyuki vitaendelea kupitiwa upya kufuatana na mahitaji na kwa ushirikiano wa karibu baina ya watafiti na watumiaji wa matokeo ya utafiti.***

Utafiti na maendeleo ya ufugaji nyuki ni mambo ambayo yatahimizwa, na rasilimali za kifedha za kutosha zitatolewa kupitia mfumo wa uchangiaji gharama, na kuanzishwa kwa mifuko ya utafiti. Mpango Mkuu wa utafiti na maendeleo ya ufugaji nyuki utatungwa kwa kushirikiana na washikadau kama vile wafugaji nyuki, watengenezaji malighafi, wafanya biashara na wawakilishi wengine wa sekta zinazoendana na hii ya ufugaji nyuki ambao wanajumuika katika maendeleo ya utafiti na maendeleo ya maliasili na kilimo. Mpango Mkuu huo utaonyesha maeneo muhimu kwa utafiti na maendeleo ya ufugaji nyuki yatakayopitiwa mara kwa mara kufuatana na kanuni ya utafiti kimahitaji. Utafiti na maendeleo ya ufugaji nyuki yatakayosisitiza kuboreshwa kwa hifadhi za nyuki na mimea ya chakula chao, usimamizi bora zaidi wa manzuki kwa kutumia aina za nyuki wa asali wa kiasili utaendelezwa. Ushirikiano baina ya asasi za utafiti utahimizwa. Uhusiano wa karibu kati ya asasi za utafiti na watumiaji utaanzishwa kwa kutumia ubadilishanaji wa habari, mikutano, semina na mipango ya pamoja ya utafiti. Ushirikiano wa kikanda na wa kimataifa katika utafiti wa ufugaji nyuki utaimarishwa.

### 4.6.6 Mafunzo na Elimu ya Ufugaji Nyuki

Habari kuhusu soko la nguvukazi kwa ajili ya ufugaji nyuki hazipo na mipango kwa ajili ya mafunzo ya watumishi haijaandaliwa kikamilifu. Aidha, kuna upungufu katika mafunzo maalum na mitaala haijafanyiwa marekebesho ili kukidhi mahitaji. Mafunzo kwa vitendo ni dhaifu na mitaala haitoi nafasi za kutosha kwa ajili ya mafunzo mahususi. Uhusiano baina ya taasisi ya mafunzo ya ufugaji nyuki na zile za sekta nyingine ni dhaifu. Kutokana na kutokuwapo kwa fedha za kutosha, Chuo cha Ufugaji Nyuki cha Tabora ambacho ni cha pekee katika nchi zote za SADC na Afrika kusini mwa Sahara hakitumiwi kikamilifu : Shughuli za kibiashara na ushirikiano wa kikanda miongoni mwa asasi za mafunzo vitahimizwa kwa lengo la kuongeza uchangiaji gharama na kujitegemea kifedha. Shughuli za kibiashara zinajumuisha: kuanzisha na kusimamia manzuki; huduma za ushauri wa kitaalam; kununua

na kuuza mazao ya nyuki; kutengeneza vifaa kwa ajili ya ufugaji nyuki na kadhalika.

***Tamko la Sera (35): Ili kuhakikisha upatikanaji wa watumishi wa kutosha wenye utaalam, ufundi na ubingwa katika sekta, mafunzo ya ufugaji nyuki yataimarishwa. Mafunzo ya ubingwa yatahimizwa.***

***Tamko la Sera (36): Ili kufanikisha maendeleo ya wafanyakazi, tathmini ya mahitaji ya nguvukazi itafanyika. Aidha, mitaala itarekebishwa na mipango ya mafunzo itaandaliwa.***

Ili kuhakikisha kuna wataalam wa kutosha wenye sifa zinazostahili kwa ajili ya kusimamia sekta ya ufugaji nyuki, rasilimali za kutosha zitatolewa kwa ajili ya kuimarisha mafunzo. Mfumo wa tathmini ya mahitaji ya nguvukazi, urekebishaji wa mitaala na utayarishaji wa mpango wa mafunzo utaanzishwa na kuendelezwa. Ushirikiano wa kimataifa katika kuendesha mafunzo ya ufugaji nyuki utahimizwa.

#### 4.6.7 Huduma za Ugani wa Ufugaji Nyuki

Huduma madhubuti za ugani ni muhimu kwa ajili ya kukuza ushirikishwaji kwa wananchi katika ufugaji nyuki-kilimo misitu. Kuna upungufu wa fedha na watumishi wa kutoa huduma za ugani katika sekta ya ufugaji nyuki na hakuna ushirikiano baina ya sekta za maliasili na kilimo. Hali hii inapelekea wananchi kupatiwa ujumbe unaopingana. Zaidi ya hayo, mitaala ya shule za msingi na sekondari haizingatii utoaji elimu ya kutosha kuhusu usimamizi wa rasilimali za maliasili.

***Tamko la Sera (37): Ili kuhakikisha kuwa kuna mwamko na stadi miongoni mwa wananchi katika usimamizi endelevu wa rasilimali za ufugaji nyuki, uwezo wa kutoa huduma za ugani wa ufugaji nyuki utaimarishwa.***

***Tamko la Sera (38): Ujumbe wa ugani wa ufugaji nyuki unaotolewa na sekta zinazosimamia maliasili na sekta nyingine husika utahuishwa kupitia mipango unganishi, utafiti na mafunzo.***

Ili kuongeza mwamko na stadi miongoni mwa wananchi katika kuhifadhi, kusimamia na kutumia rasilimali za nyuki, uwezo wa huduma za ugani utaimirishwa. juhudi za ugani zitaelekezwa kwa wafugaji nyuki binafsi, jumuiya na usimamizi wa pamoja wa hifadhi za nyuki na manzuki. Ili kuwa

na huduma madhubuti za ugani, uratibu miongoni mwa sekta utaimarishwa. Kwa kupitia mipango unganishi ya ugani, ujumbe wa ugani utazingatia jinsia.

Mtaala wa ugani wa ufugaji nyuki utarekebishwa kuzingatia matumizi mbalimbali ya rasilimali ya nyuki. Ujumbe wa ugani utatayarishwa kwa kuzingatia jiografla na ikolojia kwa kushirikiana kwa karibu na watumiaji. Mashirika yasiyo ya kiserikali na asasi nyingine zitashirikishwa katika ugani kupitia uratibu, mafunzo na utayarishaji wa vifaa. Uanzishwaji wa elimu ya mazingira na maliasili katika shule za msingi na sekondari utaungwa mkono.

### 4.6.8 Vyama vya Ushirika na Jumuiya nyinginezo za Wafugaji Nyuki.

Vyama vya Ushirika na jumuiya nyinginezo ni pamoja na; Ushirika wa Wafugaji Nyuki Tabora (TBCS), Ushirika wa Wafugaji Nyuki wa Kibondo (UKI), Chama cha Wafugaji Nyuki Tanzania (TABEA) na Chama cha Wafugaji Nyuki Arusha (ABA). Ufanisi wa vyama hivi unaathiriwa na udhaifu wa huduma za ugani, utafiti, habari za masoko na miundombinu.

***Tamko la Sera (39): Serikali itahamasisha kuanzishwa kwa vyama vya ushirika na jumuiya nyinginezo za ufugaji nyuki, na itavipatia vikundi hivi huduma za ugani, utafiti na habari za masoko.***

### 4.6.9 Biashara ya Mazao ya Nyuki

Ili kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya nyuki nchini, mfumo madhubuti wa biashara ya mazao hayo unahitajika. Mfumo wa sasa unakabiliwa na matatizo yafuatayo:

- Kutokuwapo udhibiti na ukaguzi thabiti wa ubora wa mazao;
- Kutokuwapo kwa habari za kuaminika kuhusu uzalishaji, mahitaji na bei za mazao ya nyuki;
- Kutokuwapo kwa vifaa vinavyofaa kufungia asali na nta;
- Kuuza nta na asali ghafi badala ya kuuza nta na asali iliyochakatwa;
- Wafanyabiashara wa mazao ya nyuki kutokuwa na mtaji wa kutosha wa kufanyia kazi.

Matatizo haya na mengine ndiyo yanayoleta ugumu katika kununua na kuuza mazao ya nyuki katika wakati unaofaa na kwa kiasi kinachohitajika. Hali hii huleta hasara hasa kwa wafugaji nyuki na taifa kwa jumla.

***Tamko la Sera (40): Ili kuhakikisha kwamba kuna mfumo thabiti wa biashara ya mazao ya nyuki, udhibiti wa ubora wa mazao hayo na ukaguzi utaimarishwa. Biashara ya mazao ya nyuki itahimizwa kwa kuimarisha huduma za kuaminika za udhibiti wa ubora na ukaguzi wa mazao na habari za masoko.***

### 4.6.10 Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo yanahusiana na sekta ya ufugaji nyuki na ambayo yanashiriki katika kuhifadhi na kusimamia rasilimali za nyuki, ni yale ambayo yanajihusisha na kupanda mimea ya chakula cha nyuki, kununua na kuuza mazao ya nyuki, kuhifadhi wanyamapori, nyuki na maliasili kwa ujumla.

Katika shughuli za ufugaji nyuki, Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanaweza kuwafikishia wafugaji nyuki, wakulima na jumuiya, ushauri wa ugani na motisha nyinginezo. Hata hivyo mashirika hayo yana upungufu wa nguvukazi na fedha. Kutokuwapo kwa uratibu miongoni mwa mashirika hayo kunapelekea kufanya shughuli zinazofanana katika eneo moja.

***Tamko la Sera (41): Uratibu na ushirikiano kati ya sekta ya ufugaji nyuki na mashirika yasiyo ya kiserikali vitaimarishwa.***

Uratibu baina ya sekta ya ufugaji nyuki na mashirika yasiyo ya kiserikali vitaimarishwa. Kuanzishwa kwa mashirika yasiyo ya kiserikali mapya na ushiriki wake katika maandalizi ya mipango na programu zinazohusiana na ufugaji nyuki vitahimizwa. Aidha, mashirika yasiyo ya kiserikali yatahimizwa yajiimarishe na kujitegemea kifedha ili kujihakikishia uendelevu wake.

### 4.6.11 Masuala ya Fedha

Maendeleo ya sekta ya ufugaji nyuki yametawaliwa na utegemezi mkubwa kwa wahisani na fedha za umma. Mbinu za sekta kujitosheleza kifedha hazijaendelezwa. Uchumi dhaifu na riba kubwa vimekwamisha kupata fedha za kutosha za ndani. Fedha kutoka sekta binafsi ni kidogo kutokana na kukosekana kwa utaratibu mzuri wa upatikanaji wake. Zaidi ya hayo baadhi ya taratibu za utoaji fedha za kimataifa zilizopo kama vile "badili deni kwa mali" hazijatumiwa na serikali ambayo hata hivyo imeshindwa kukusanya fedha za kutosha kukidhi masharti yaliyopo. Tatizo hili pia linapelekea nchi kushindwa kutekeleza wajibu wake wa kimataifa wa makubaliano na mikataba mbalimbali. Aidha, baadhi ya programu zinazoendeshwa kwa misaada kutoka nje zimeshindwa kuweka misingi ya kuiwezesha serikali kuziendeleza programu hizi mara uhisani unapokwisha.

***Tamko la Sera (42): Taratibu mpya na bunifu za upatikanaji wa fedha kisekta zitaanzishwa na kuelekezwa kwenye shughuli za msingi za washikadau katika sekta ya ufugaji nyuki.***

Sera mpya imejengeka katika misingi ya uanzishwaji wa mifumo ya kujitosheleza kifedha, kama vile taasisi za utekelezaji na michango zaidi ya sekta binafsi na ya wananchi. Taratibu za kitaifa na ngazi za vijiji za kupata fedha za kujitosheleza kwa uwekezaji wa sekta binafsi na wananchi kwa jumla kwenye shughuli za ufugaji nyuki zitaendelezwa. Kujitosheleza kifedha kwa sekta ya umma pia kutatiliwa mkazo kwa njia ya tathmini ya rasilimali kwa kupanga bei inayozingatia thamani halisi kiuchumi na ukusanyaji mzuri wa mirabaha na ada nyinginezo.

Shughuli zifuatazo zitaendelezwa kama mkakati wa kujitegemea kifedha:-

- Kununua na kuuza asali na nta;
- Utengenezaji na uuzaji wa vifaa kwa ajili ya ufugaji nyuki;
- Kutengeneza na kuuza bidhaa zitokanazo na asali na nta;
- Kutoza ada ya uchavushaji wa mazao,
- Kutoza ada ya kiingilio katika hifadhi za nyuki na manzuki;
- Kutoza ada ya huduma ya kuondoa nyuki wasumbufu-,
- Kuuza vitabu, majarida, magazeti na machapisho mengineyo yahusuyo ufugaji nyuki n.k.

Taratibu za muda mrefu za kupata fedha kwa ajili ya utafiti wa ufugaji nyuki kwa kushirikiana na jumuiya ya kimataifa zitaendelezwa. Ili kuongeza uwezo wa kujitosheleza kifedha, baadhi ya shughuli za utafiti zitaendeshwa kibiashara. Uchangiaji wa gharama za mafunzo kwa watumiaji mbalimbali na uendelezaji wa shughuli za kibiashara na za vyuo vya mafunzo kwa njia ya kuinua kiwango cha kijitosheleza kifedha vitaanzishwa. Utoaji wa mafunzo na huduma za elimu kibiashara katika maeneo maalum kama vile viwanda vinavyojikita kwenye ufugaji nyuki vitahimizwa.

Uchangiaji wa gharama utaimarishwa ili kuboresha huduma za ugani. Mashirika yasiyo ya kiserikali pia yatahimizwa kuendesha shughuli za biashara ili kujihakikishia uendelevu.

Vyombo vya utoaji fedha vilivyopo ikiwa ni pamoja na vya umma na binafsi vitatumiwa kikamilifu. Fedha zinazotolewa na wahisani zitaunganishwa kwenye mifumo ya kitaifa ya utoaji fedha na mazingira mazuri yatajengwa ili fedha hizo zitumike kuinua uwekezaji katika sekta binafsi.

Mifumo ya muda mrefu ya upatakanaji fedha kutoka nje ya nchi kwa ajili ya miradi yenye umuhimu kimataifa kama vile ya uhifadhi na utafiti itaendelezwa. Mifumo hii itahusika kuwa na mifuko ya fedha ya uhifadhi na utafiti.

### 4.6.12 Jumuiya ya Kimataifa

Tanzania ni mwanachama wa mashirika ya kimataifa ambayo yanafanya utafiti kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya ufugaji nyuki kama vile Chama cha Kimataifa cha Utafiti wa Nyuki (IBRA) ambacho makao yake makuu ni Uingereza na Chama cha Kimataifa cha Umoja wa Wafugaji Nyuki (APIMONDIA). Kutokana na uhaba wa fedha za kigeni Tanzania inashindwa kulipa ada ya uanachama ya kila mwaka na michango mingine ya vyama hivyo.

Mipango itafanywa baina ya Tanzania na vyama hivyo ili ada za uanachama na michango mingine viweze kulipwa kwa njia ya mazao ya nyuki kama nta na asali. Kwa sasa vyama hivyo vinakubali michango ya ada ya uanachama kwa kutumia mazao ya nyuki.

Pamoja na nafasi muhimu ya misaada ya fedha ya kimataifa kwa sekta ya ufugaji nyuki, uratibu wa wahisani katika sekta hii bado hauridhishi. Kipaumbele cha baadhi ya wahisani wakati mwingine hakilingani na kile cha Tanzania. Aidha, watumishi wengi wenye ujuzi wameacha kazi kwenye sekta ya umma kutokana na kuvutiwa na mishahara mizuri katika miradi inayopata uhisani kutoka nje. Baadhi ya miradi inayopata misaada ya kifedha kutoka kwa wahisani imejitengenezea mifumo sambamba na ile ya serikali na hali hii imeleta matatizo na wasiwasi katika mahusiano yake na serikali.

***Tamko la Sera (43): Ili kuepuka kuwa na programu zinazolingana na kuingiliana, mashauriano na wahisani kuhusu uratibu wa miradi au programu yataimarishwa.***

***Tamko la Sera (44): Wawekezaji kutoka nje watahimizwa kuwekeza katika programu na miradi ambayo wafugaji nyuki na wafanya biashara wa hapa nchini hawawezi kumudu.***

Mfumo unaofaa wa utaratibu wa wahisani katika sekta ya ufugaji nyuki utaanzishwa. Miradi inayopata misaada ya kifedha toka kwa wahisani itaingizwa katika mipango ya serikali.

## 5. DHIMA NA MAJUKUMU YA WASHIKADAU WAKUU.

Dhima na majukumu ya Washikadau Wakuu katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ni kama ifuatavyo:

| DHIMA YA MSHIKADAU | UANZISHAJI NA USIMAMIZI ENDELEVU WA HIFADHI ZA NYUKI NA MANZUKI | VIWANDA VINAVYOJIKITA KWENYE UFUGAJI NYUKI NA MAZAO | UFUGAJI NYUKI KATIKA MAENEO YA SEKTA MTAMBUKA KWA AJILI YA UHIFADHI NA USIMAMIZI WA MIFUMO YA IKOLOJIA |
|---|---|---|---|
| **1** | **2** | **3** | **4** |
| 1.Wafugaji nyuki, wakulima na jumuiya za wananchi | • Uhifadhi na usimamizi wa nyuki wa asali na mimea ya chakula chao katika vijiji na hifadhi za nyuki binafsi.<br>• Uanzishaji na usimamizi wa hifadhi za nyuki za vijiji.<br>• Ushiriki katika usimamizi wa pamoja wa hifadhi za nyuki.<br>• Kuchagua sehemu za kuanzisha manzuki.<br>• Utengenezaji wa vifaa vya ufugaji nyuki.<br>• Mizinga kupata makundi ya nyuki.<br>• Kuanzisha manzuki.<br>• Kuwalinda nyuki dhidi ya moto, wadudu/ wanyama waharibifu na viuwadudu.<br>• Kuzalisha na kuchakata mazao ya nyuki kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.<br>• Kuanzisha na kusimamia manzuki katika makazi ya watu.<br>• Uundaji na utekelezaji wa sheria ndogondogo.<br>• Kuanzisha na kusimamia manzuki katika maeneo yaliyohifadhiwa.<br>• Kuajiri watumishi kwa ajili ya usimamizi wa manzuki na matumizi ya mazao ya nyuki. | • Uzalishaji wa mazao na bidhaa za nyuki kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na biashara.<br>• Ajira katika viwanda vya ufugaji nyuki.<br>• Kuweka viwango vya ubora wa mazao ya nyuki.<br>• Kudumisha Viwango vya Ubora wa mazao ya nyuki kwa ajili ya soko la kimataifa. | • Kutumia bomba la moshi, mavazi ya kinga pamoja na mizinga inayofaa ili kuimarisha uhifadhi endelevu wa mifumo ya ikolojia.<br>• Kuhifadhi na kupanda mimea ya chakula cha nyuki.<br>• Uanzishaji na usimamizi wa mfumo wa ufugaji nyuki kilimo misitu. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2.Sekta binafsi na/au taasisi za utekelezaji. | • Usimamizi wa pamoja wa hifadhi za nyuki.<br>• Utoaji wa ajira.<br>• Uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za nyuki na mimea ya chakula chao kwa kutumia mavazi ya kinga, bomba la moshi na mizinga sahihi.<br>• Kuhamasisha na kutoa huduma za ugani.<br>• Kugharimia uwekezaji katika sekta ya ufugaji nyuki.<br>• Kutangaza mazao ya nyuki na kukuza masoko yake. | • Kutoa ajira.<br>• Kuzalisha bidhaa zinazotokana na mazao ya nyuki kama vile mishumaa, bia, mvinyo, vitu vitamu, vipodozi, polishi, mafuta ya kulainisha n.k.<br>• Kuendeleza mazao na masoko.<br>• Uwekezaji katika teknolojia ya uzalishaji isiyoharibu mazingira.<br>• Kuhamasisha na kutoa huduma za ugani.<br>• Kugharimia uwekezaji katika viwanda vya ufugaji nyuki.<br>• Kuendeleza utalii wa kiikolojia katika sekta ya ufugaji nyuki. | • Usimamizi wa pamoja wa hifadhi za nyuki.<br>• Kutoa ajira .<br>• Uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za nyuki na chakula chao kwa kutumia mavazi ya kinga, bomba la moshi na mizinga sahihi.<br>• Kuhamasisha na kutoa huduma za ugani.<br>• Kugharimia uwekezaji katika sekta ya ufugaji nyuki.<br>• Kutangaza mazao ya nyuki na masoko yake.<br>• Kutumia miongozo ya Bioanuwai katika kusimamia shughuli za ufugaji wa nyuki.<br>• Kutumia ukadiriaji wa athari kwa mazingira kwenye uwekezaji katika sekta ya ufugaji nyuki.<br>• Kutumia mabadiliko ya idadi ya nyuki wasiouma kama kiashirio cha hali ya mazingira.<br>• Usimamizi wa pamoja wa maeneo yaliyohifadhiwa. |
| 3. Serikali za mitaa. | • Uratibu wa huduma za ugani wa ufugaji nyuki na sekta nyingine zinazohusiana.<br>• Kukusanya mapato.<br>• Kusimamia utekelezaji wa sheria.<br>• Kusimamia manzuki za maonesho.<br>• Kuanzisha, kusimamia na kuendesha hifadhi za nyuki.<br>• Kufuatilia maeneo ya hatimiliki za manzuki.<br>• Usimamizi wa pamoja wa hifadhi za nyuki na manzuki za maonesho. | • Urekebishaji/Udhibiti.<br>• Kukusanya mapato. | • Urekebishaji/Udhibiti.<br>• Usimamizi wa pamoja wa hifadhi za Nyuki.<br>• Usimamizi wa pamoja wa manzuki za maonesho.<br>• Uratibu wa huduma za ugani wa ufugaji wa nyuki na sekta nyingine zinazohusiana. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4.Serikali kuu. | • Uundaji wa sera.<br>• Uandaaji wa Mipango na bajeti za sekta.<br>• Kuandaa sheria.<br>• Kusimamia utekelezaji wa sheria.<br>• Ukusanyaji wa mapato.<br>• Usimamizi wa hifadhi muhimu za nyuki.<br>• Ufuatiliaji na tathimini.<br>• Mifumo ya utoaji wa habari.<br>• Mipango ya uendelezaji wa nguvu kazi.<br>• Huduma za ugani.<br>• Utafiti na uratibu wake.<br>• Mafunzo na kuendeleza mitaala.<br>• Uratibu wa washikadau wengineo.<br>• Ushirikiano wa kimataifa. | • Uundaji wa sera.<br>• Uandaaji wa mipango na bajeti za sekta.<br>• Kuandaa sheria.<br>• Kusimamia utekelezaji wa sheria.<br>• Ufuatiliaji na tathimini.<br>• Mifumo ya utoaji wa habari.<br>• Mipango ya upatikanaji na uendelezaji wa nguvu kazi.<br>• Huduma za ugani.<br>• Utafiti na uratibu wake.<br>• Mafunzo na kuandaa mitaala.<br>• Uratibu wa washikadau wengineo.<br>• Ushirikiano wa kimataifa. | • Uundaji wa Sera.<br>• Uandaaji wa mipango na bajeti za sekta.<br>• Kuandaa sheria.<br>• Kusimamia utekeleza wa sheria.<br>• Ufuatiliaji na tathimini.<br>• Mifumo ya utoaji wa habari.<br>• Mipango ya upatikanaji na uendelezaji nguvukazi.<br>• Huduma za ugani.<br>• Utafiti na uratibu wake.<br>• Mafunzo na Kuendeleza mitaala.<br>• Uratibu wa washikadau wengineo.<br>• Ushirikiano wa kimataifa. |
| 5.Jumuia ya Kimataifa | • Mshirika katika maendeleo endelevu.<br>• Kutoa misaada kifedha.<br>• Kujenga uwezo kupitia misaada ya kiufundi; mafunzo na uhawilishaji teknolojia.<br>• Kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Kimataifa. | • Mshirika katika maendeleo endelevu.<br>• Kutoa misaada kifedha.<br>• Kujenga uwezo kupitia misaada ya kiufundi; mafunzo na uhawilishaji teknolojia.<br>• Kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Kimataifa. | • Mshirika katika maendeleo endelevu.<br>• Kutoa misaada kifedha.<br>• Kujenga uwezo kupitia misaada ya kiufundi; mafunzo na uhawilishaji teknolojia.<br>• Kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya kimataifa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6. Taasisi Nyingine za Kiserikali. | • Uratibu na Ushirikiano katika ugani, mafunzo na utafiti.<br>• Kusimamia utekelezaji wa sheria.<br>• Kutoa msaada katika ufuatiliaji na tathmini.<br>• Kusaidia uhifadhi wa nyuki na mimea ya chakula chao.<br>• Kusaidia katika Ukusanyaji na usambazaji wa habari.<br>• Ufuatiliaji wa matumizi ya ardhi. | • Uratibu na Ushirikiano katika ugani, mafunzo na utafiti.<br>• Kusimamia utekelezaji wa sheria.<br>• Kutoa msaada katika Ufuatiliaji na tathmini.<br>• Kusaidia uhifadhi wa nyuki na mimea ya chakula chao.<br>• Kusaidia katika ukusanyaji na Usambazaji wa habari.<br>• Ufuatiliaji wa matumizi ya ardhi.<br>• Kutoa msaada katika utoaji wa leseni za viwanda na biashara. | • Uratibu na<br>• Ushirikiano katika ugani, mafunzo na utafiti.<br>• Kusimamia utekekelezaji wa sheria.<br>• Kutoa msaada katika ufuatiliaji na tathmini.<br>• Kusaidia uhifadhi wa nyuki na mimea ya chakula chao.<br>• Kusaidia katika ukusanyaji na usambazaji wa habari.<br>• Ufuatiliaji wa matumizi ya ardhi. |
| 7.Mashirika yasiyo ya Kiserikali. | • Kuhamasisha na kutoa huduma za ugani.<br>• Kujenga uwezo wa kiutendaji.<br>• Msaada wa Mafunzo na kiufundi.<br>• Kugharimia ufugaji nyuki na uhifadhi wa mazingira.<br>• Kukuza majukumu ya kijinsia na kuwapa uwezo wanawake.<br>• Kuwahamasisha vijana washiriki katika shughuli za ufugaji nyuki. | • Kuhamasisha na kutoa huduma za ugani.<br>• Kujenga uwezo wa kiutendaji.<br>• Msaada wa Mafunzo na kiufundi.<br>• Kugharamia ufugaji nyuki na uhifadhi wa mazingira.<br>• Kukuza majukumu ya kijinsia na kuwapa uwezo wanawake.<br>• Kuwahamasisha vijana washiriki katika shughuli za ufugaji nyuki. | • Kuhamasisha na kutoa huduma za ugani.<br>• Kujenga uwezo wa kiutendaji.<br>• Msaada wa mafunzo na kiufundi.<br>• Kugharamia ufugaji nyuki na uhifadhi wa mazingira.<br>• Kukuza majukumu ya kijinsia na kuwapa uwezo wanawake.<br>• Kuwahamasisha vijana washiriki katika shughuli za ufugaji nyuki. |

A:sera ya taifa ya ufugaji nyuki/seranyu.doc